Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 183 | MUHR./SAFAR 1437 AH | OKT./NOV. 2015 | TABK./ NUBW. 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa; na kwa yakini Allah Anao uwezo wa kuwasaidia. Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wanasema: Mola wetu ni Allah. Na kama Allah Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Allahu hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Allah Humsaidia yule anayemsaidia Yeye; hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mshindi; (22:40-41)

Jalsa Salana ya 46 Tanzania yafana

Mahudhurio juu na Huduma bora

Na Mwandishi wetu, Dar es Salaam

Jalsa Salana ya 46 Tanzania imemalizika kwa mafanikio makubwa huku kukiwa na mabadiliko mengi ya mahudhurio na huduma.

Jalsa hiyo ilifanyika siku za Ijumaa hadi Jumapili tarehe 2 - 4 Oktoba 2015 kwenye viwanja vya Jumuiya Kitonga, kata ya Msongola, Ilala Dar es Salaam. Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. alituma salamu maalum kwa ajili ya Jalsa salana hiyo. (*Salamu hizo zipo uk. 5*).

Jalsa salana ya mwaka huu imekuwa na mafanikio makubwa hasa kwenye upande wa mahudhurio ambapo zaidi ya wanajamaat 3600 kutoka sehemu mbalimbali nchini walihudhuria. Pia Wanajumuiya kutoka Msumbiji na Malawi nao walihudhuria Jalsa hiyo. Jambo lingine lililoonesha mabadiliko makubwa kwenye Jalsa ya mwaka huu ni uborekaji wa huduma mbalimbali. Maboresho hayo ni pamoja na kuezekwa kwa sehemu ya Jalsa Gah kwa kinamama na hivyo kutoa nafasi kubwa zaidi ya makazi. Pia kwa kupatikana umeme wa kutosha wa mwanga wa jua, huduma za maji, taa na vipaza sauti pia nazo ziliboreka.

Amir na Mbashiri Mkuu Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akifungua Jalsa hiyo aliwakaribisha wageni wote na kuwashukuru kwa kujitolea muda wao wenye thamani na kugharimika kwa ajili ya kuhudhuria mkutano huo wa kidini.

Aidha aliwakumbusha kwamba Sayyidna Ahmad as,

Endelea uk. 2



Amir na Mbashiri Mkuu Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akifungua mkutano wa mwaka 2015 Kitonga Dar es Salaam

Jihadi aliyopigana Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika kuitetea Islam

Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa 2015 na Sheikh Waseem Ahmad, Mwanza

Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema Mwingi wa Ukarimu

Ndugu zanguni wapendwa,mada niliyopangiwa kuizungumzia siku hii ya leo ni jihadi aliyopigana Masihi Aliyeahidiwa as katika kuitetea Islam.Ndugu wasikilizaji,hii ni suna na desturi ya Allah Subhanahu wa Taala ya kuwa Yeye Hutuma mitume wake duniani ili waweze kuihami na kuitetea dini yake ili dini ile istawi na kuimarika na iweze kuwa sehemu ya maisha ya watu ya kila siku na mwishowe binadamu waweze kumtambua Mwumba wao na kuishi maisha ya kitawa.

Sasa mitume hao wafikapo,wapo wanaowaamini na kuwakubali na kujiunga nao,lakini wengine pamoja na kuwakataa kata kata huonesha upinzani mkali,huwapinga na kutengeneza hila tofauti kwa lengo la kuwaangamiza na kuharibu kazi yao na huongezeka katika kuwapinga manabii hao kwa kiasi hiki kuwa kusudio lao la kuishi duniani kunakuwa kuwamaliza tu.

Katika hali kama hiyo Allah Subhanahu wa Taala Ambaye Ndiye Mweza na Mwenye jalali Husimama pamoja na waja wake na Huwasaidia na kuwahami na Huonesha shani yake ya ajabu kwa ajili yao na kutokana na ahadi yake isemayo KATABALLAHU LAAGHLIBANNA ANA WA RUSULI yaani Allah Amekwishaandika kuwa bila shaka yoyote Nitashinda Mimi na Mitume wangu. Anasimamisha mja wake kwa ajili ya kuitetea dini yake na Humsaidia na kuweka mkono wake juu yake na hivyo tukio la ajabu linatokea ambapo malaki ya wafu huhuika na wanaokuwa wameharibika tangu vizazi hata vizazi huzishika khulka za Mungu na vipofu huanza kuona na midomo ya mabubu huanza kueleza maarifa ya Mwenyezi Mungu na mara moja mapinduzi yale yanapatikana duniani ambayo hakuna jicho linakuwa limeyaona hapo kabla wala sikio lolote linakuwa limeyasikia.

Ndugu wapendwa hivyo ndivyo itokavyo miaka elfu moja mia nne iliyopita wakati jua la ukweli lilipotoka kutoka farani na dunia ikamtambua Mwumba wake na Islam ilipata ushindi ulio wazi,tena Mwenyezi Mungu Alimtuma msidikishaji wa WA AAKHARIINA MIN HUM Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad as wa Qadian Akimfanya kuwa Masihi na Mahdi wa zama hizi ili tauhidi yake ipatikane duniani tena na ukweli wa Bwana wetu Mtukufu na nuru ya Qurani Tukufu idhihirike duniani.

Ndugu wasikilizaji,Bwana wetu Mtukufu Hadhrat Muhammad Mteule saw alipotoa bishara ya Hadhrat Imam Mahdi na Masihi as,akaeleza pia kuhusu kazi zake zilizokuwa zimeunganishwa naye asemapo atakayeishi mionogoni ni mwenu atapata kuonana na isa bin mariamu akiwa imamu mahdi ,mwamuzi mwadilifu ambaye atavunja msalaba na kuua nguruwe, MUSNAD AHMAD.

Katika hadithi hii Bwana wetu Mtukufu saw alitufahamisha kuwa wakati ule uislamu utakuwa umedhoofika kiasi hiki kuwa umma wake utakuwa umefanana na mayahudi.Usalaba utapata nguvu na binadamu asili mia kubwa watakuwa wameiga sifa za nguruwe.

Ndugu waislamu sawa na bishara hiyo tunapoangalia zama zile alipodhihirika na kufika duniani Hadhrat Ahmad as Imam mahdi na Masihi aliyeahidiwa, dini tukufu ya Islam ilikuwa imezungukwa na mashambulio ya watu wa dini zote. Katika uwanja huu wa kuishambulia dini tukufu ya Islam ukristo ulikuwa umewashinda wengine na ulikuwa kwenye safu ya kwanza katika kazi hii.

Kuipinga Islam, kuikashifu, kuleta tuhuma juu ya Bwana wetu Mtukufu, kuandika vitabu vichafu pamoja na kuwadanganya na kuwapotosha waislamu wasiokuwa na elimu ya kutosha, hayo yote yalikuwa mambo yao ya kutenda kila siku.

Mapadre wao kwa kinagaubagha walikuwa wakiwapotosha waislamu wa kawaida wakisema kwao "Masihi aliye hai na yupo mbinguni ni sehemu ya imani yetu

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Ahadi ni Deni

Wakati wa uchaguzi mkuu hewa nzima ya taifa letu ilijaa bidhaa mja adhimu. Bidhaa hiyo ni ahadi. Masikio yalichoka kwa wingi wa ahadi na vichwa vilitafakari juu ya ahadi hizo. Ahadi hizo zilifanana na sentensi ndefu isiyo na kituo. Tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu ya kwamba kipindi hicho tumekimaliza salama. Tunaweza kujihesabu kwamba kipindi hicho tumekimaliza. Na sasa tunaingia katika ingwe ya pili ambayo ni utekelezaji wa ahadi tulizozitoa kwa wananchi.

Sawa na utaratibu wa jamii yetu 'ahadi ni deni' na deni siku zote lazima lilipwe. Na wanaodaiwa ni wale ambao walitoa ahadi. Na wanaodai utimizaji wa ahadi hizo ni wale waliofurika viwanjani huku jua likiwawakia wakiwa wanawasikiliza watoa ahadi. Kama ahadi hizo zilikuwa ni daraja la kuwavusha watoa ahadi ili waende ng'ambo ya pili ya uongozi hiyo itakuwa bahati mbaya na msiba mkubwa kwa taifa letu. Ni dhahiri muda mwingi ulitumika kwenda kuwasikiliza watoa ahadi. Watoa ahadi nao walijitayarisha, wakachapisha ahadi zao, wakazunguuka ili kufikisha ahadi zao kwa wananchi. Vyombo vya habari havikuwa nyuma, vilipeperusha ahadi hizo. Wengine walikwenda mbali Zaidi, wakawatafuta hata wasanii ilimuradi ujumbe wao uweze kufika.

Matarajio yetu ni kwamba wale watoa ahadi wanawajibu wa kuzipitia kwa uangalifu ahadi zote walizozitoa na kuziwekea mikakati ya utekelezaji ahadi hizo. Ni dhahiri ya kwamba 'Ada ya mja kunena, muungwana ni vitendo'. Safari hii kuliko wakati wowote mwingine katika historia yetu tunatarajia utekelezaji wa ahadi na tueleze utekelezwaji huo hatua kwa hatua.

Sawa na mafundisho ya Islam, ahadi ni mkataba, ni makubaliano, ambayo unatakiwa Inshallah uyatekeleze. Zito Zaidi ni kwamba usipofanya hivyo kuna siku utaulizwa. Na wakati wa kuulizwa ni mgumu sana kwani ni wakati huo huo pia hukumu inapotolewa.

Uwanja upo wazi kwa viongozi wetu kutimiza ahadi zao. Fursa ya kufanya mambo yaliyoahidiwa kutekelezwa ipo, na matatizo na kero za wananchi ni nyingi sana. Na bila shaka kuna utamu mkubwa unapopata fursa ya kutatua kero za binadamu wenzio. Ni katika mnasaba huu basi kama tungelikuwa na uwezo tungeshauri kila kiongozi asome kwa uangalifu sana maisha ya Khalifa wa pili wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) Seyyidna Umar bin Khatab (ra) ambaye wakati wake wote alitawaliwa na hofu ya Allah. Alielewa vilivyo kwamba kila tendo alilokuwa anatenda gizani au penye mwanga Allah Alikuwa Anamuona. Huu ni mtazamo chanya na unaweza kumsaidia kiongozi kuchukua tahadhari. Seyidna Umar (ra) katu hakusubiri taarifa zinazoletwa mezani kwake, yeye alikwenda mwenyewe na wakati mwingine bila kujitambulisha ili kufahamu matatizo ya raia wake. Ni kiongozi aliyesimamia haki bila upendeleo wowote. Myahudi na Muislam walikuwa na tatizo lao na wakaenda kwake na akampa haki Myahudi. Yeye na mtumishi wake walikubaliana ya kwamba wapande farasi kwa zamu na ilipotokea kwamba wanaingia mjini mtumishi alimwambia kiongozi wa Waaminio ingawaje hii ni zamu yangu, panda wewe watu watanifikiriaje. Khalifa Umar (ra) alisema hatuwezi kuvunja mkataba kwa sababu ya kuhofu binadamu. Waliingia mjini mtumishi yuko juu ya farasi na kiongozi wa dola akiwa anatembea kwa miguu.

Seyidna Umar (ra) alikuwa Mshairi mzuri na aliyefahamu mashairi mengi kwa ghaibu. Moja ya ubeti wake maarufu unasema; Hufurahi sana napoletewa zawadi katika kikapu kilichojaa udhaifu wake. Hakukasirika hata kidogo kukosolewa. Kwa hakika alifurahia sana kukosolewa. Kwani alifahamu vilivyo kuwa hakuna binadamu aliyekamilika. Kuwa tayari kukosolewa ni jambo ambalo hujenga uhasama katika sehemu zetu hizi za Afrika. Huu ni utamaduni unaoweza kutusaidia sana katika Afrika. Kuwa tayari kukosolewa. Kuhimili wimbi linaloonesha udhaifu wako na kuwashukuru wale waliokukosowa ni dalili nzuri ya maendeleo. Seyidna Umar (ra) hakusubiri hata kidogo labda iwepo sababu maalum, kutochukua hatua kwa haraka iwezekanavyo. Alikuwa ni kiongozi anayeamini kwamba hatukuwa na muda mwingi hapa duniani na hivyo ilitakiwa tufanye mambo yetu kwa haraka tukielewa kwamba muda haukuwa upande wetu.

Kuwapa watu matumaini katika jamii, katika jambo ambalo huwezi kulitekeleza, hilo kwa Seyidna Umar aliona ni kosa kubwa. Yeye aliamini kwamba usiwape watu matumaini ambayo unaelewa fika huwezi kuyatekeleza.

Limekuwepo kosa la kuamini kuwa kama ilivyo vigumu kwa tembo kupita kwenye tundu la sindano hivyo hivyo ni vigumu mafundisho ya Islam yakawekwa katika vitendo. Maisha ya Seyidna Umar (ra) ni somo kwetu sisi sote kwamba unaweza kuyatekeleza mafundisho ya Islam ukijaaliwa kupata fursa ya kuongoza watu. Ndiyo maana mwanzoni tulisema, pangekuwepo na uwezekano kila kiongozi kabla hajala kiapo asome na kuyaelewa maisha ya Seyidna Umar (ra) ambaye ni nuru katika ulimwengu wa siasa uliojaa giza.

Jalsa Salana ya 46 Tanzania

Kutoka uk. 1

Masihi na Mahdi aliyeahidiwa a.s. alipowaarifu wafuasi wake kwa mara ya kwanza juu ya mpango huu wa Jalsa Salana kwa idhini ya Allah, aliwaelezea madhumuni yake hasa' akisema:
"Lengo na shabaha ya Jalsa Salana ni kuwakusanya pamoja mara kwa mara wanajamati, wakutane kuleta mabadiliko ndani mwao ili mioyo yao ielekee kwenye maisha ya Akhera, wapate kumwogopa Mwenyezi Mungu, wawe mifano mizuri kwa wengine katika utawa, ucha mungu, huruma kwa wanadamu na ili uchaji Mungu upate kuongezeka katika mioyo yao. (Ushahidi wa Qurani).

Pia Amir sahib aliwakumbusha wageni wa Jalsa kwamba safari moja Hazrat Ahmad a.s akieleza umuhimu usio wa kawaida wa Jalsa Salana akasema "Jalsa hii msiichukulie kama mikutano mingine ya kawaida ya watu, hili ni jambo ambalo msingi wake umewekwa juu ya kuisaidia haki na kutangaza mafundisho sahihi ya Islam. Jiwe la msingi la silsila hii Ameliweka Mwenyezi Mungu Mwenyewe; na Ameyatayarisha mataifa yatakayokuja hivi karibuni kujiunga nayo; kwani hili ni tendo la Yule Mwenye nguvu na uwezo, Ambaye mbele yake hakuna jambo linaloshindikana.'' (Ishtehaar 7 Disemba 1892).

Wataalamu kadhaa wa Jumuiya wakiwemo masheikh, walimu na viongozi wengine walitoa mada mbalimbali sawa na ratiba ya Jalsa.
Mada zilizoongelewa ni pamoja na: Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ni Dhirisho lililo wazi la uwepo wa Mwenyezi Mungu; Jihadi aliyopigana Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika kuitetea Islam; Muongozo wa Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. juu ya Tabligh na Tarbiyyat; n.k.

Kama ilivyo ada kila kikao kilifunguliwa kwa usomaji w Quran tukufu na mashairi yaliyoghaniwa kwa sauti nzuri. Pia nafasi zilitolewa kwa Atfal na Nasirat kughani mashairi kwenye Jalsa hiyo.
Miongoni mwa wageni waalikwa waliofika kwenye Jalsa hiyo ni Bw. Ramadhani Mapuri ambaye alimwakilisha Mwenyekiti wa kituo cha Haki za binadamu na utawala bora na Bw. Shaaban Saidi Mdumila ambaye alimwakilisha Mh. Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam.

Katika salamu zao viongozi hao wote wawili waliishukuru Jumuiya kwa kuandaa mkutano huo katika hali ya amani pamoja na kuzishirikisha taasisi za kiserikali ili kushirikiana pamoja nao. Kimsingi wote waliahidi kutoa ushirikiano unaostahili katika kufanikisha malengo ya Jumuiya ambapo kaulimbiu yake ni "Mapenzi kwa wote, chuki si kwa yeyote.

Kiongozi mwingine aliyehudhuria ni Katibu Mkuu wa kanisa la Seventh Day kanda ya Kusini Mashariki Pastor Habert Mzigu ambaye alifuatana na uongozi wa kanisa hilo lilopo Temeke Dar es Salaam.

Katika salamu zake kwenye mkutano huo, kiongozi huyo aliushukuru uongozi wa Jumuiya kwa kumualika kwenye mkutano huo na kukiri kwamba hii ni mipango na mapenzi ya ya Mungu ambaye anatuwezesha watu wa imani tofauti kuweza kukaa pamoja na kutambuana ili kukuza mahusiano mema miongoni mwa wanadamu.
Pia kiongozi huyo alisema:
"Jumuiya hii iko mstari wa mbele kabisa katika kulaani na kukomesha vita na umwagaji damu wowote ule kwa jina la Uislamu. Alieleza kufarijika kwake kwa kubaini kuwa Jumuiya ya Ahmadiyya ni moja ya Jumuiya inayoongoza miongoni mwa Jumuiya nyingi za Kiislamu katika kupinga ugaidi na utumiaji nguvu wa aina zote na kusisitiza kwa vitendo kamba "Jihadi ya Upanga haina nafasi katika Uislamu leo.

Alisema kwamba leo duniani hisia zimejengeka kote kuwa Waislamu ni watu hatari sana (kiasi kwamba akionekana mtu mwenye kanzu yake, kofia kichwani/kilemba na kidevu kilichoota vizuri, watu wanakaa naye kwa tahadhari)

Hivyo akatumia nafasi hiyo kamshukuru Mungu ambaye ameruhusu kuwe na Jumuiya hii katikati ya machafuko tunayoyashuhudia, Jumuiya inayojipambanua kwa vitendo kuwa ipo kwa ajili ya kumletea binadamu Maadili, Haki na Amani.

Katika hotuba yake ya ufungaji wa Jalsa hiyo Amir sahib aliwakumbusha wale wote waliohudhuria kuhakikisha kwamba wanatekeleza kwa matendo yale yote walioyokumbushwa kwenye hotuba mbalimbali katika kipindi kizima cha mwaka kilichobaki, jambo moja kubwa likiwa umoja na upendo miongoni mwetu:

Pia akasema Hadhrat Ahmad as, Masihi na Mahdi aliyeahidiwa amekuja kuondolea mbali hitilafu, mfarakanao na utengano wa waislamu na kuwajumuisha pamoja chini ya bendera ya Mtume Muhammad saw kama asemavyo mwenyenwe: " Mimi nimekuja na mambo mawili, la kwanza ni kwamba shikeni Umoja wa Mwenyezi Mungu na la pili ni kwamba mpendane na kuhurumiana wenyenwe kwa wenyenwe. Onyesheni mfano mzuri wa namna hii kiasi hiki kwamba uwe muujiza kwa watu wengine.

Hivyo Amir sahib aliwaasa wanajumuiya na wote waliohudhuria kwamba hivi leo, Hablullah (kamba ya Allah) ambayo tunapaswa kuishika kwa nguvu zote na kufungamana nayo kikamilifu ni dhati tukufu ya Khalifa tul Masihi, Hazrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a. ambaye ni nuru ya Mwenyezi Mungu katika zama hizi za giza totoro, anayetuangazia na kutuongoza kwenye njia iliyonyooka ya Mwenyezi Mungu. Baraka na neema zote zimo katika kumpenda Khalifa Mtukufu na kumsikiliza na kumfuata barabara kwa sababu yeye ndiye mwakilishi na mpendwa wa Mwenyezi Mungu katika dunia hii ambaye atatupeleka karibu na Allah. Hivyo basi kila mmoja wetu ajitahidi kusikiliza hotuba za Khalifatul Masihi na kuyafauata yale yote yasemwayo ili aweze kuongoka na kuokoka.

Akimalizia hotuba yake na kabla ya maombi ya ufungaji, Amir sahib alimnukuu tena Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliyewaombea washiriki wa Jalsa Salana kama hivi: " Yeyote atakayefunga safari hii kwa ajili ya Mwenyezi Mungau, Mungu Awe pamoja naye, na Amlipe ujira mkubwa, Amrehemu na Amhurumie, Ampunguzie hofu na wasiwasi na Amtatulie matatizo yake, Amwondolee huzuni, Amuepushe na kila shida inayomkabili, Amfungulie milango ya miradi yake yote. Siku ya malipo Amuinue pamoja na watu waliofadhiliwa na rehema zake, na mwisho wa safari Awe khalifa wao. E Mungu, Mwenye utukufu na Mpaji, Mrehemevu na Mtatuzi wa matatizo, yapokee maombi yote haya. Utushindishe juu ya wapinzani kwa kuonesha alama za wazi wazi, kwani nguvu na uwezo vyote ni Vyako." Amen.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Mafundisho yaliyo Bora kabisa

Kutoka Maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Hadhrat Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

.... Basi mwombapo msiombe kama watu wategemeao vitu vya duniani na wanakuwa wajinga na uwezo wa Mungu, wao wametengeneza kanuni ya viumbe wenyewe ambayo haikusadikishwa na kitabu cha Mungu. Hakika wao wamekasirikiwa, na dua yao haikubaliwi. Wao ni vipofu si wenye macho wafu si wazima. Wanaweka mbele ya Mwenyezi Mungu kanuni waliyoifanya wenyewe na wanapima kwa kiasi chao uwezo wa Mungu usioweza kuhesabika wala kukusanywa; na wanafahamu kuwa Mwenyezi Mungu ni dhaifu. Basi wanatendewa na Mungu kama hali yao. Lakini unaposimama wewe kusali na kuomba ni wajibu kwako kumfahamu Mungu wako ana uwezo juu ya kila kitu; ukifanya hivi dua yako itakubaliwa na wewe utaona ajabu ya uwezo wa Mungu kama sisi tulivyoona. Na kushuhudia kwetu ni kwa kuona si namna ya masimulizi. Itakubaliwaje dua ya yule mtu, na itakuwaje moyo wake kupata ushujaa wa kuomba dua wakati taabu kubwa inapomfikia, anayeifahamu kuwa ni kinyume cha kawaida na asiyeamini kuwa Mungu ana uwezo juu ya kila kitu?

Lakini ewe mtu mwema! Wewe usifanye hivi, maana Mola wako ni yule aliyezitundika nyota zisizohesabika bila nguzo na aliyeumba mbingu na ardhi bila chochote. Je, wewe unamdhania vibaya kuwa Yeye atashindwa na haja yako? Hasha! Bali utakosa kupata bahati yako kwa sababu ya dhana yako mbaya. Ajabu za Mungu wetu ni nyingi wala hazihesabiki, lakini wanaweza kuziona wale waliojitoa kwa Mwenyezi Mungu kwa ukweli na uaminifu. Yeye hazionyeshi ajabu zake kwa watu wasioamini uwezo wake, wala watu wasio waaminifu wa kweli. Bahati gani mbaya ya mtu yule asiyejua kuwa ana Mungu mmoja Mwenye uwezo juu ya kila kitu! Hakika pepo yetu ni Mungu wetu na ladha yetu yote ni kwa Mola wetu. Sababu sisi tumemwona na tumeukuta kila uzuri ndani Yake. Inafaa kujipatia hazina kama hii hata kwa kutoa roho. Na inafaa kununua almasi hii hata kwa kutoa uzima wote. Enyi wenye bahati ndogo! Kimbilieni upesi kwenye chemchemi hii ambayo itawanywesheni! Ndiyo chemchem ya uzima itakayowalindeni! Nifanye nini na niingize namna gani mioyoni mwenu maneno haya ya furaha? Kwa ngoma gani ninadi katika masoko kuwa Mola wenu ni huyu ili watu wasikie? Na niwape dawa gani ili masikio ya watu yafunguke na yasikie?

Kama ninyi mtakuwa wa Mungu, fahamuni kwa yakini kuwa Mwenyezi Mungu pia atakuwa wa kwenu. Mkiwa mmelala, Mwenyezi Mungu Atawalindeni. Mkiwa mmeghafilika juu ya adui zenu Mwenyezi Mungu Atawaangalieni na atavunja hila zao. Mpaka sasa hamjajua uwezo wa Mungu wenu, lau kama ninyi mngalijua haya isingetokea siku yoyote ninyi kuhuzunikia dunia yenu. Mtu mwenye hazina akipoteza pesa moja analia au anapiga kelele au anajiangamiza? Basi lau kama mngalijua habari za hazina hii, ya kwamba Mungu wenu anaweza kuwasaidieni katika kila wakati wa haja msingalihangaika kupenda dunia. Mwenyezi Mungu ni hazina ipendwayo, iheshimuni. Yeye ndiye msaidizi wenu katika kila mahali. Ninyi si kitu pasipokuwa Yeye, wala vitu vyenu wala hila zenu.

Msifuate mataifa yaliyoangukia na kutawakali juu ya vitu na hila zao. Wao wamekula udongo wa vitu vya dunia kama nyoka anavyokula udongo. Na kama mbwa na mbesi wanavyokula nyamafu, hivi ndivyo wao wameuma nyamafu. Wamekuwa mbali sana na Mwenyezi Mungu! Wamewaabudu watu na wamekula nguruwe na wametumia pombe kama maji. Na wamehilikishwa kwa sababu ya kuangukia kwao kwenye vitu na kuacha kuomba nguvu kwa Mungu. Na roho ya mbinguni imeruka kutoka kwao kama njiwa anavyoruka kutoka katika kiota. Katika mioyo yao mna ukoma wa kupenda dunia, uliovikata viungo vya ndani yao vyote. Basi jihadharini na ugonjwa huu! Mimi siwakatazeni kutumia vitu, bali nawakatazeni msiwe kama mataifa mengine waliokuwa watumwa wa vitu tu, na kumsahau anayeumba vitu kama anavyoumba viumbe vingine. Lau kama mnayo macho mngaliona kuwa hapana kitu chochote ila Mwenyezi Mungu tu. Wala hamwezi kunyosha mikono yenu wala hamwezi kuikunja ila kwa idhini Yake. Mfu wa roho atalicheka, laiti angalikufa ingalikuwa bora kuliko kucheka kwake!

Jihadharini! Msifuate mataifa mengine baada ya kuona hali yao kwamba wao wameendelea mbele katika hila yao ya dunia, kwa hiyo na sisi pia tuwafuate nyayo zao, hapana! Sikilizeni na fahamuni, kwamba wao hawamfahamu Mwenyezi Mungu yule anayewaiteni kwake maana wamemsahau. Je, mnajua Mungu wao ni nani? Hakuwa ila ni mtu dhaifu! Kwa hivi wametumbukizwa katika kughafilika. Mimi siwakatazeni kuchuma na kutafuta manufaa ya dunia; lakini ninawaambieni kuwa msiwafuate wale wanaofahamu kuwa dunia ni peke yake. Bali ni lazima juu yenu kumwomba Mungu Mwenyezi ili awapeni nguvu siku zote katika kila kitendo kama kitendo cha dunia au kitendo cha dini. Mwombeni uwezo na nguvu siku zote si kwa midomo tu, bali inafaa kwenu kuamini kwa yakini kwamba baraka zote zinatoka mbinguni tu. Mtakuwa wakweli mtakaposhika njia hii, yaani katika kila kitendo na kila taabu kabla ya kushika shauri lolote, fungeni mlango wenu na kiangukieni kizingiti cha Mwenyezi Mungu na ombeni kwake kwa unyenyekevu; Ee Mola wetu, tumepata taabu hii, kwa fadhili zako tuondolee. Ndipo roho takatifu itateremka kwenu kuwasaidieni na wakati ule mtafunguliwa njia ya msaada kwa siri. Jirehemuni nafsi zenu wala msiwafuate wale waliokataa kufungamana na Mungu na kuangukia vitu vya dunia hata hawasemi Inshallah (Mungu Akipenda) kwa kupata nguvu.

Mwenyezi Mungu ayafumbue hasa macho yenu ili mjue kuwa Mungu wenu ndiye nguzo za mashauri yenu yote; na kama nguzo zikianguka, jee paa linaweza kukaa? La, bali litaanguka mara moja, na inamkinika kuwaua watu wengi. Hivi ndivyo haiwezekani kuendelea mashauri yenu sawasawa bila msaada wa Mwenyezi Mungu. Na kama ninyi hamtaomba msaada kwake, wala hamtafanya desturi zenu kuomba uwezo kwake, hamtapata ufaulu kabisa. Na mwishoni mtakufa kwa majuto makubwa.

Msidanganywe kuwa kwa nini mataifa mengine, wasiomjua Mungu ambaye ndiye Mungu wenu Mkamilifu na mwenye uwezo, wanaendelea mbele na kustawi? Majibu yake ni haya; kuwa mataifa haya kwa sababu ya kumwacha Mwenyezi Mungu wameingizwa katika mtihani wa dunia. Mtihani wa Mungu baadhi ya wakati unakuwa hivi; yaani anayemwacha Mungu na kupenda utamu na ladha ya dunia na matamanio yake, na anataka mali ya dunia; basi anafunguliwa milango ya mali ya dunia na akawa tajiri; lakini katika dini anakuwa maskini na uchi kabisa, na mwisho wake anakufa katika mazoea ya dunia na kutupwa motoni. Lakini wakati mwingine mtihani unakuwa hivi ya kuwa ananyang'anywa katika dunia pia na hapati chochote. Lakini mtihani wa namna hii hauna maumivu sana kama mtihani wa kwanza, kwani mwenye mtihani wa kwanza anakuwa na kiburi sana kuliko mwenye mtihani wa pili. Lakini pamoja na haya hawa wote wawili wanakasirikiwa na Mungu. Kwa sababu Mwenyezi Mungu ni chemchem ya hali ya furaha ya kweli kweli, ikiwa wao wanamsahau Mungu Mzima wa milele, na si haya tu bali pia hawamjali na wanatokana naye, itamkinikaje kwao kupata hali ya furaha ya kweli? Hubarikiwa anayeifahamu siri hii na huangamizwa asiyeifahamu siri hii.

Vile vile mnatakiwa msishike njia ya mafilosofa (philosophers) wa kidunia wala msiwatazame mtazamo wa heshima, kwani madhana yao yote ni ya upumbavu. Hekima ya kweli ni ile aliyowafundisheni Mwenyezi Mungu katika maneno yake. Wamekwishaangamia wale wenye kupenda hekima ya kidunia na wamestawi wale wenye kutafuta elimu ya kweli na hekima katika kitabu cha Mungu. Kwa nini mnachagua njia za upumbavu? Je, mnamfundisha Mungu asiyoyajua? Lakini hekima ya kweli mlioahidiwa inapatikana kwa roho takatifu. Ninyi kwa msaada wa roho takatifu mtafikishwa kwenye elimu yenye kuchipusha moyo na kuuhuisha na kuufikisha kwenye mnara wa yakini. Anayekula nyamafu atawaleteeni wapi chakula chema? Na mwenye kuwa kipofu atawezaje kuwaongozeni? Kila hekima tukufu inatoka mbinguni, basi mnatafuta nini kwa hao watu wa ardhini? Hakika hao waendao roho zao mbinguni wamekuwa warithi wa hekima. Unatakiwa utakasifu wa moyo, na ukweli na kujitakasa – baada ya haya yote, hekima ya kweli na elimu tukufu na utulivu mtapata.

Sikilizeni! Msidhani kuwa ufunuo wa Mwenyezi Mungu umekwisha zamani na hautakuja . Wala msiseme kwamba roho takatifu (Jibril) hatateremka tena bali aliteremka zamani tu. Kweli kweli nawaambieni; milango yote inafungwa, lakini mlango wa kuteremkia roho takatifu haufungwi kabisa. Fungueni milango ya roho zenu ili aingie roho takatifu. Hakika ninyi mnajitupa mbali na jua mnapofunga dirisha la kuingilia nuru yake. Ewe mwenye akili ndogo! Simama, ufungue dirisha ili jua liingie ndani yako. Ikiwa kama Mungu hakuwafungieni njia za baraka za dunia siku hizi bali amewazidishieni, jee, mnadhani kuwa amewafungieni njia za baraka za mbinguni ambazo siku hizi mnazo haja nazo sana? Hasha! Bali umefunguliwa mlango ule wazi kabisa. Sasa kama Mungu Amewafungulieni moango wa neema na baraka zote za kwanza kwa kufuatisha mafundisho yake aliyofundisha katika sura ya Alhamdu, kwa nini mnakataa kuzipokea neema na baraka hizi? Kuweni wenye kiu kwa sababu ya chemchem hii na maji yatakuja yenyewe kwenu. Lilieni maziwa, kama mtoto anavyolili maziwa ya mama yake, na maziwa yatachuruzika yenyewe. Wezeni kurehemu, ili mrehemiwe. Onyesheni mahangaiko, ili mpate utulivu.

Lilieni mara kwa mara ili mshikwe na mkono mmoja. Ni njia yenye taabu namna gani, iliyo njia ya Mungu! Lakini n jia hii hufanywa nyepesi kwa wale wanaojitupa katika shimo la taabu kwa nia ya kufa. Hao wanaohukumu katika mioyo yao kuwa 'tunakubali moto na tutaungua kwa ajili ya Mpenzi wetu Mwenyezi Mungu', kisha wao hujitumbukiza katika moto kumbe moto ule ni pepo. Na hivi ndivyo alivyosema Mungu katika Kurani Tukufu; "Wain minkum illa waariduha kana 'alaa Rabbika hatman maqadhiyya' (Sura 19 aya 72) - Enyi watu wabaya na wazuri, hapana yeyote kwenu asiyepita kwenye moto wa jahannam, lakini hao wanaounguzwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wataokolewa katika moto. Lakini yule mwenye kuunguzwa kwa ajili ya nafsi yake yenye kumwamrisha kutenda mabaya, basi moto utamwunguza.

Amebarikiwa yule mwenye kupigana na nafsi yake kwa ajili ya Mungu. Na bahati mbaya kwa yule anayepigana na Mungu kwa ajili ya nafsi yake, wala asipatane naye. Mwenye kuvunja amri ya Mungu kwa ajili ya nafsi yake haingii katika ufalme wa mbinguni kabisa. Kwa hiyo jitahidini ninyi msishuhudiwe hata na herufi au nukta moja ya Kurani khilafu zenu ili msikamatwe kwa sababu yake. Maana, hata shari kidogo inaleta adhabu. Wakati ni kidogo na mwendo ni mrefu, nyanyueni upesi upesi nyayo zenumaana usiku umekaribia. Na kile mnachotaka kumpelekea kitazameni marakwa mara ili kisipunguke kitu cho chote na kupunguka huku kusije kuwasababu ya hasara yenu; au visije kuwa vitu vyote vibaya au vibovu ambavyohavifai kupelekwa zawadi katika baraza la Mfalme wa Wafalme.

Safina ya Nuhu

Itaendelea toleo lijalo. Inshallah

Jihadi aliyopigana Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kutoka uk. 1

nanyi pia mnakubali hilo.Sisi pia tunamsubiri yeye na nyinyi vile vile mnamngoja aje kuwaongoza nyinyi waislamu. Sasa basi mbona mnasubiri nini,njooni muungane nasi na badala ya kumwamini Yesu Kristo kwa kesho atakapoteremka mbinguni afadhali mumkubali leo, na karibuni mupande safina hii ambayo nahodha wake yuko hai.

Ndugu watukufu, matokeyo yake yaliyodhihirika yalikuwa ya kutisha sana.Wakati huo malaki ya waislamu walijitenga na kuiacha dini tukufu ya islam na wakajiunga na Ukristo. Miongoni mwa hao walikuwa na baadhi ya masheikh wakubwa wakubwa nao pia wakatangaza kuwa kuanzia siku ile badala ya kutajwa kuwa masheikh wa kiislamu watajwe mapadre wa kikristo, mmoja wao alikuwa Sheikh Emaad ud deen wa Ajmer ambaye alikuwa Imamu wa msikiti mkuu wa Ajmeer, yeye alijiunga na Ukristo na hakuishia hapa tu bali alionesha upinzani mkali kuhusu Islam naye akaandika vitabu vingi vikieleza tuhuma na kashfa dhidi ya Islam.

Ndugu zangu wapendwa, msifikiri kuwa upinzani huu ulikuwa umeishia hapa hapa bali mbali na hapo mtandao wake ulikuwa umeenea hadi Ulaya ambapo mapadre kama vile padre lifrae na wenziye walikuwa wakipanga mipango mbali mbali ya kuiangamiza Islam pamoja na fikra na madai kuwa dini itakayofuatwa duniani ni dini yao ya Ukristo,

Katika vita hii ya kuiangamiza islam mabaniyani, makasinga na mayahudi vile vile wakachangia mchango wao na wakaandika vitabu vingi vikimpinga islam na mtume wake, jambo hili halikwishi hapa tu bali upande wa pili hali ya waislamu ilikuwa kama inakuwa mtoto yatima akiwa ameachwa njiani bila kupewa msaada wowote. Viongozi wa dini ya islamu ambao ilikuwa wajibu wao kuitetea islamu na kuwajibu wapinzani wake walikuwa wamekosa nguvu,nao walikuwa taswira ya hadithi ya Bwana wetu Mtukufu isemayo, Ni karibu iwadie juu ya watu zama ambapo hakitabaki chochote cha Islam isipokuwa jina lake wala hakitabaki chochote cha Qurani isipokuwa maandishi yake. Katika zama hizo misikiti yao itaendewa kidhahiri na watu wengi lakini itakuwa mitupu upande wa mwongozo; maulamaa wao watakuwa wabaya sana kuliko wowote walio chini ya mbingu. Kutoka kwao fitina itatokea na itawarejea wao wenyewe.

HALI hii ilikuwa inamwudhi sana roho ya Hadhrat Ahmad as,akielezea hali na uchungu wa moyo wake anasema katika shairi yake ya kiajemi

1-Dini ya Ahmad imekuwa haina msaidizi, hakuna aliye rafiki yake. Kila mtu yumo katika shughuli zake, haijali dini ya Ahmad saw.

2-Mafuriko ya upotevu yamechukua malaki ya wanadamu na kutupa kila upande. Ole wake jicho lisilozinduka hata sasa.

3-Enyi waislamu, tupeni jicho kwenye hali ya dini hata mara moja.Mabalaa niyaonayo, hamna haja ya kuyaeleza.

4-Moyo wangu kila saa unafurukuta katika damu, hakuna ayajuaye maumivu yetu minghairi ya Mjuzi wa siri.



Umati uliofurika kwenye mkutano wa mwaka 2015 - Kitonga Dar es Salaam

5-Naona damu ya dini ikitiririka kama waliouawa huko Karbalaa. Ni ajabu kuwa watu hawa hawana huba ya Mpenzi huyu.

6-Tazama jinsi dini isiyo na kifani chini ya mbingu inavyogaragara vumbini kwa kudhulumiwa na watu waovu.

7-Ewe Allah usiufurahishe ule moyo wenye giza, usiojali dini ya Ahmad Mteule saw.

Kisha kuhusu masingizio yaletwayo na wakristo juu ya nabii wetu mtukufu Hadhrat Masihi Mauud as anasema kuwa, Mapadre wa kikristo wamezua mengi juu ya Mtume wetu saw. Hakuna kitu kilichoniudhi roho yangu zaidi kuliko hayo maneno ya dhihaka na masihara wanayotunga wao juu ya mtakatifu mtume wetu huyu.

Moyo wangu umejeruhika kwa sababu ya hao kumkashifu na kumwaibisha mbora wa viumbe.

Haki ya Mungu,kama watoto wangu wote na wajukuu wangu na vilembwe vyangu na marafiki zangu na wasaidizi wangu wote wauwawe mbele ya macho yangu hata mimi mwenyewe nikatwe mikono na miguu,na mboni za macho yangu kutolewa nje wala nisipate muradi wangu hata mmoja, tena ninyimwe furaha na starehe zangu zote. SHIDA hizi zote SI kitu zikilinganishwa na msiba wa mtume wetu mtukufu saw kufanyiwa mashambulio machafu. EWE mola wetu uliye mbinguni utuhurumie na kutusaidia na kutuokoa na mtihani huu.

Hivyo katika hali hiyo wakati imani ilipokuwa imetungikwa kwenye kilimea, kwa amri ya Allah Subhanahu wa Taala Hadhrat Syedna Ahmad as alitangaza ilani ya kupigana jihadi dhidi ya kila mpinzani wa Islam na sawa na mahitaji ya zama zile akawatangazia kupigana jihadi kwa kalamu yake. SAFFE DUSHMAN KO KIYA HUM NE BAHUJJAT PAMAAL. SEIF KA KAAM QALAM SE HI DIKHAYA HUM NE

Katika kazi zake, kazi moja ilikuwa kazi ya kuwajibu maswali na tuhuma ziletwazo na wapinzani wa Islam na wakati huo huo pia kulikuwa na kazi ya kuwaongoza waislamu kwenye njia iliyonyoka na kuwaelimisha elimu hoja na dalili.

Ndugu wasikilizaji, Syedna Ahmad as kwa kuuona uislamu umekuwa shabaha ya mashambulio machafu toka pande zote na hali ya waislamu kurudi nyuma, imani kupisha dhana na dini kuwa kitu cha juu juu tu,yeye alijitia katika kazi ya kuueleza Uislamu, kwanza kabisa alitunga kitabu chake kiitwacho Barahine Ahmadiyya na kuwatangazia wote kuwa Islam ni dini yenye uzima ambayo kwa kuifuata, mtu angeweza kupata mwungano na Mola wake na kuingia katika mazungumzo naye.

Kitabu hiki kilileta mapinduzi katika uwanja huu wa kupigana jihadi kwa kalamu.Ndani ya kitabu hicho Hadhrat Ahmad as alijadili kwa kina sana juu ya haja ya ufunuo na ukweli wake, ukweli wa Islam, ubora wa kurani Tukufu, qudra ya Allah na elimu yake yenye wasaa, uumbaji wa Allah na nguvu zake za umiliki, ilmuradi kwa kuandika kitabu hiki adhimu akathibitisha ubora wa Islam juu ya dini zote.

ISLAM SE NA BAGHO RAHE HUDA YAHI HA, EE SONE WALO JAGHO SHAMSU DHUHA YAHI HA.

MUJ KO QASM KHUDA KI JIS NE HAMEN BANAYA,ABB AASMAN K NICHE DINE KHUDA YAHI HA Molvi Muhammad Husein wa Batala ambaye alikuwa kiongozi maarufu wa dhehebu la Ahli hadithi aliandika katika gazeti lake la Ishaatusunna,akasema kuwa: kwa rai yetu katika zama hizi na kwa kuangalia hali ya sasa ilivyo, hiki ni kitabu ambacho ndani yaIslam mpaka sasa hakijawahi kuchapwa. Kwa maoni yetu na kwa hali ilivyo ndani ya Islam hakuna kitabu kilichowahi kuandikwa chenye hadhi kama hiki.

Mwandishi wake pia amethibitisha kuwa msaidizi wa Islam kwa mali, kwa kalamu na kwa nafsi kiasi kwamba MFANO WAKE unapatikana kwa waislamu wachache tu waliopita zamani.

Kitabu hiki kilikuwa cha kwanza kilichoandikwa na Syedna Ahmad as katika kuitetea Islam na kuihami dini tukufu ya Allah na siku za badaye zilishuhudia askari huyu wa Allah, Masihi wa zama akiwa pekeyake akipigana jihadi kwa kalamu yake na vitabu vyake zaidi ya themanini na tano katika lugha tofauti na hutuba zake na mijadala yake aliyoifanya na wakristo,mabaniani na waislamu ni ushahidi mmoja kati ya shahada nyingi juu ya ukweli huu kuwa YEYE ndiye aliyekuwa Jarriullah, simba wa Mungu, ambaye alipewa jina la SULTANUL QALAM na Allah Aliipa kalamu yake jina la Zulfiqaar Ali na akasema kuwa kuna siri yake humo ya kuwa zama hizi ni zama za kupigana jihadi kwa kalamu.

Ndugu wasikilizaji, Hadhrat Ahmad as katika maandishi yake mara kwa mara aliamsha hisia za waislamu ili waelewe hali ya dini na wajibu wao.

Sehemu moja alisema "ENYI Waislamu watafutao ukweli na wapenzi wa kweli wa Islam, iwe wazi kwenu kwamba zama hizi tunamoishi ni zama za giza ambamo mambo yote,yawe ya kiimani au ya kimatendo yamechafuka sana na upepo mkali wa upotevu unavuma kutoka kila upande. Kitu kiitwacho imani, kimekuwa ndiyo maneno matupu yanayotamkwa kwa ulimi na mila chache au ubadhirifu na shuguli za kujionyesha zimefahamika kuwa ndiyo mambo yanayoitwa matendo mema. Kisha Syedna Ahmad as alisema

Mafundisho ya wakristo pia yanatayarisha mashimo mbalimbali ya baruti kulipua ukweli na uaminifu. Na wakristo kwa kufutilia Islam, wakizusha njia zote za kisiri za uwongo na uzushi,kwa juhudi kubwa kabisa wanazitumia kwa kunyanganya na mbinu mpya mpya za kudanganya na njia mpya za kupoteza zinaundwa. Na wanafedhehesha mtu mkamilifu aliye fahari ya watakatifu wote na taji la watawa wote na mwongozi wa mitume wote watukufu hata kwamba katika tamasha mbali mbali sura za islam na mwongozi mtakatifu wa islam zinaonyeshwa kwa njia mbaya na michezo ya kuigiza huonyeshwa na tuhuma za kiuzushi zinaenezwa kwa njia ya majumba ya michezo ambamo ushenzi wote umetumiwa kwa kufedhehesha islam na Nabii Mtukufu saw.

Hivyo basi kwa kubatilisha uwongo wao na kwa kudhihirisha ukweli wa dini yake,Allah Amemtuma mtumishi wake huyu kukabiliana na wapinzani kwa kumjaalia ufunuo wake na maongezi yake na Baraka zake maalum na kumpatia sehemu kamili ya elimu za ndani za njia yake.

Basi Enyi wenye busara, msione ajabu kwamba Mwenyezi Mungu katika wakati wa haja na katika siku hizi za giza totoro, Ameteremsha nuru ya mbinguni na kumtuma mtu mmoja duniani kwa kumteua kwa masilahi ya watu wote na kwa shabaha ya kuishindisha Islam na kueneza nuru ya yule aliye mbora wa viumbe vyote na kwa kuwatilia nguvu Waislamu, na pia kwa ajili ya kutakasa hali yao ya ndani. Ajabu ingekuwa kama Mungu Aliye Mlinzi wa dini ya Kiislamu Ambaye Aliahidi kwamba daima Nitakuwa Mwangalizi wa mafundisho ya Qurani na Sitayaacha yadhoofike tena kufifia na kupoteza nuru yake, kwa kuona giza hili na ufisadi wa ndani na nje Angekaa kimya wala Asingekumbuka ahadi Yake. Basi si jambo la ajabu bali ni la kutoa shukurani mara elfu kwa elfu na ni wakati wa kuongeza imani na yakini kwamba Mwenyezi Mungu kwa fadhili na ukarimu wake ametimiza ahadi yake na hakuahirisha hata kwa dakika moja kutimiza bishara ya mtume wake.

Ndugu wasikilizaji Hadhrat Ahmad as alifanya mijadala mingi na wakristo na Mwenyezi Mungu Alimjaalia kupata ushindi ulio wazi. Nependa kuweka mbele yenu mfano wake mmoja, mjadala mmoja uliofanyika mjini Amratsar. Tukio moja la ajabu lilitokea nalo ni hili kuwa kwa vile Hadhrat Masihi Mauud as alikuwa amedai kuwa yeye yu mfano wa Masihi Issa bin Mariyam na imeelezwa ndani ya Biblia kuwa Masihi alikuwa akiwaponya wagonjwa kwa kuwagusa tu. kwa hiyo siku ile padre mmoja aliwaleta walemavu watatu wanne na vipofu, akawaficha upande fulani,zamu yake ilipofika ya kutoa mada, hapo akawatoa wale walemmavu na akamdai Hadhrat Masihi Mauud as kuwa wewe si unasema kuwa U mfano wa Masihi, sasa walemavu hawa wachache wako mbele yako. Ebu uwaponyeshe kwa kuwagusa tu.

Ndugu zanguni, hapo baadhi ya waliohudhuria wakaanza kucheka,hata baadhi ya wajumbe wa mkutano pia wakapata hofu, wakahamanika kwamba kwa njia ya kielimu jibu lake litapatikana, lakini hali hii kwa dhahiri inaonyesha kuwa wapinzani wamepata nafasi ya kulifanyia mzaha. Hata hivyo Hadhrat Ahmad as alikaa kwa utulivu na amani, alijua kuwa Mkono wa Mungu upo juu yake naye sawa na ahadi yake Atamsaidia na kudhihirisha ukweli wa Islam na Atawafedhehesha maadui zake.

Kisha zamu yake ya kuongea ilipofika,simba huyu wa Mungu aliinua na kusema kuwa, Mimi katika hali hii sikubaliani na

Endelea uk. 5

Jihadi aliyopigana Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Kutoka uk. 4

miujiza ya Masihi Issa bin Mariyam na simaanishi kama wamanishavyo Wakristo, nami kwa dhati yangu pia sidai jambo hili kuwa kwa kutaka kwangu naweza kumponyesha mgonjwa kwa kumgusa tu, hivyo basi haiwezekani kuniomba mimi jambo ambalo ni kinyume na ninavyoamini, lakini hata hivyo hakuna shaka kuwa ndani ya agano jipya Hadhrat Issa bin Mariyam kwa vyovyote aliwaambia wafuasi wake kuwa kama nyinyi ndani yenu mtakuwa na imani sawa na punje ya haridari, nyinyi mtaweza kuiambia milima iondoke sehemu moja iende sehemu nyingine na hakuna jambo lolote linaloweza kushindikana kwenu.

Mimi nina yakini kuwa Wakristo waliokusanyika hapa,bila shaka wana imani ya kweli juu ya Masihi Issa bin Mariyam na bila shaka imani yenu ni kubwa kuliko punje ya haridali, hivyo mimi nawashukuruni kuwa nyinyi mmeniondolea usumbufu wa kuwakusanya wagonjwa na kuwaleta hapa, haya basi zawadi yenu mliyoleta hii hapa, wako mbele yenu, hebu waguseni ili muthibitishe imani yenu.

Watazamaji wanasema kuwa jibu hili la Hadhrat Masih Mauud as likawachanganya na kuwafanya wababaike na wakaanza kuwaficha wagonjwa walemavu huku na kule na mchezo huu ukawarudia wao wenyewe na lile jambo walidai kuwa ni ushindi wao likabadilika kuwa ni kushindwa kwao.

Ndugu Waahmadiyya, mfano mwingine ni tukio lile litokalo mnamo mwaka 1896 wakati Allah Taala Alimjaalia Syedna Ahmad as kuwa mwakilishi wa Islam katika mkutano wa dini uliokusanya dini mbali mbali na Akamjaalia kupata ushindi juu ya dini zote. Mkutano huu wa dini ulifanyika mjini Lahore mnamo tarehe 26 hadi 29 Desemba mwaka 1896. Mkutano huu uliitishwa na kiongozi mmoja wa kibaniani Swami Shugan Chandar, aliyesema kwamba shabaha ya mkutano ni kwamba, ili iamuliwe dini ipi imejaa ukweli mtupu.

Syedna Ahmad as alipendekezwa na Waislamu wengi kwamba aiwakilishe Islam katika mkutano huo. Syedna Ahmad as alipoalikwa na wasimamizi wa mkutano alikubali kwa moyo wote mwito huu na akaandika makala ambayo ilisomwa mkutanoni na sahaba wake mmoja maarufu Maulawi Abdul Karim Sialkoti ra. Siku chache kabla ya mkutano kufanyika Syedna Ahmad as alitangaza kwa njia ya karatasi zilizochapishwa na kuenezwa nchini kote kwamba Mwenyezi Mungu Amemwambia kwamba "MAKALA HII ITAZISHINDA MAKALA ZOTE ZINGINE"

Bishara iliyotolewa naye ilitimia ajabu. Watu wote kwa sauti moja walitamka baada ya kusikiliza makala hii kwamba kwa kweli makala hii imezishinda makala zote zingine. Magazeti yaliisifu sana mno makala hii bali yakaandika kwamba makala zingine kwa kulinganishwa na makala hii hazikuwa chochote wala lolote.

Gazeti la GENERAL wa Gauhar Asifii likaandika katika toleo lake la tarehe 24 Januari 1897, Ni kweli kabisa kwamba kama si makala ya Hadhrat Mirza Sahib, Waislamu wangedhalilika na kujuta mbele ya wafuasi wa dini zingine. Lakini Mkono wenye nguvu wa Mungu Uliihami dini tukufu ya Kiislam isianguke, bali kwa njia ya makala hiyo Islam ikapata ushindi hata kwamba achilia mbali marafiki, maadui nao wakatamka kwa jazba ya kitabia kwamba makala hii imezishinda makala zote,imezishinda makala zote.Bali makala ilipomalizika kusomwa maadui wakakiri wakisema:sasa uhakika wa Islam umebainika na Islam imepata ushindi. Ndugu katika imani, kazi moja nyingine iliyofanywa na Syedna Ahmad as ambayo ni mfano unaongaa kama nyota huku mbinguni ni kuonesha shani ya kipekee ya kurani Tukufu kwa waislamu na wengine. Hadhrat Masihi Mauud as alitangaza kuwa mawazo ya waislamu wa sasa kuwa elimu



Sheikh Waseem Ahmad, akitoa hotuba kwenye Jalsa Salana 2015

za kurani Tukufu zimeishia kwa wanazuoni waliopita na kwamba yale waliyoyasema au waliyoyaandika ndiyo mwisho wa maelezo ya kurani Tukufu, HAYA ni mawazo potofu naye akaandika kuwa Mwenyezi Mungu Ameniambia kuwa kama vile dunia hii kwa dhahiri ni ulimwengu wa maada ambamo sawa na haja ya kila zama hazina ya kimaada huwa inapatikana, VIVYO HIVYO Qurani Tukufu ni ulimwengu wa kiroho ambapo hazina za ulimwengu wake wa kiroho na kielimu hazitakwisha kamwe na kufuatana na haja za kila zama zitaendelea kupatikana.

Yeye alidai kuwa kwa vile Mwenyezi Mungu Ameniteua mimi kuitumikia kurani Tukufu hivyo basi mimi ndiye niliyepewa ufahamu wa kurani Tukufu ambao katika zama za leo hakuna yeyote mwingine aliyepewa ufahamu huu nami nimepewa nguvu hii kuwa kulingana na haja za zama hizi nieleze elimu na hazina za kurani Tukufu, niziweke mbele ya watu ambao hapo awali hazikuweza kubainishwa na kwa wito wa nguvu akaandika kuwa katika zama hizi katika jambo hili HAKUNA mtu yeyote anayeweza kushindana nami.

Ilmuradi yeye aliandika mara kwa mara na kuwaita watu kwa nguvu kuwa kama kuna mtu yuko mwenye ubavu basi aje mbele yangu ashindane nami katika kuandika maelezo ya kurani Tukufu lakini hakuna aliyepata ujasiri wa kujitokeza kushindana na Hadhrat Masih Mauud as.

Tena Akawatolea wito huu mara kadhaa kwa viongozi wa dini zingine pia kuwa waje kwake washindane naye waeleze ubora wa maarifa ya mafundisho yao kutoka ndani ya vitabu vyao vya dini zao naye ataeleza ukweli na ubora wa kurani Tukufu. Kisha itapimwa kuwa kitabu cha nani kina maarifa bora zaidi na chenye hazina ya ukweli na kipi si cha kweli LAKINI hata hivyo hakuna mtu yeyote aliyeitikia wito wake.

Ndugu wapendwa hapa naweka mbele yenu rai iliyotolewa na baadhi ya wapinzani wa jumuiya juu ya kifo cha Hadhrat Imam Mahdi as ambayo inathibitisha wazi kuwa Syedna Ahmad as jinsi alivyopigana jihadi katika kuitetea Islam kwa maisha yake yote hata watu wasiokuwa na wafuasi wake nao pia wakalazimika kukiri kwamba huyu ndiye aliyetimiza haki ya kuwa mwakilishi wa Islam.Gazeti moja liitwalo 'CURZEN GAZZETTE' Mhariri wake Mirza Heerat Dehlevi aliandika kuwa; "Utumishi wa hali ya juu wa marehemu aliofanya kuihami Islam dhidi ya Maariya na Wakristo kwa kweli unastahili sifa kubwa sana. Yeye alibadili kabisa mwelekeo wa mihadhara ya kidini na alianzisha mtindo mpya kabisa wa maelezo ya vitabu nchini India. Si kama Muislam bali kwa kuwa watafiti wachunguzi, sisi tunakiri jambo hili kuwa Padri yeyote mkubwa au kiongozi yeyote mkubwa hakuwa na ujasiri wa kufungua mdomo mbele (dhidi) ya marehemu Mirza Ghulam; ingawa marehemu alikuwa Mpanjabi lakini ndani ya kalamu yake mlikuwa na nguvu kiasi hiki kwamba leo nchini hakuna mwenye uwezo wa kuandika yenye nguvu kama yeye, nguvu ya maandishi yake yalikuwa ya kipekee katika shani yake. Ni kweli kabisa kuwa baadhi ya maandishi yake yakisomwa yana leta hali ya ulevi wa kiroho moyoni. Yeye amepitia katika mioto ya bishara za maangamio. Yeye amepitia ndani ya maangamio ya upinzani na mioto ya hoja za watoa hoja na akasafisha njia yake na akafikia kilele cha maendeleo yake ya juu sana" .

Mhariri wa gazeti lisilokuwa la Waahmadiyya "WAKIL" aliandika kuwa; "Mtu yule alikuwa mtu mkubwa sana, ambae kalamu yake ilikuwa sihir na ulimi wake ulikuwa uchawi, mtu yule aliyekuwa mwili (umbo) wa bongo za maajabu, ambae (macho-maono) yake yalikuwa majaribio na sauti yake ilikuwa ya kutisha (mfano wa sauti itakayotolewa siku ya kiyama). Ambaye vidole vyake vilikuwa vimezuungushwa na unganishwa na nyaya za mapinduzi, na ambae viganja vyake viwili vilikuwa mawe mawili ya betri. Mtu huyo ambae kwa muda wa miaka thalathini amekuwa kimbunga na tetemeko katika dunia ya kidini,kifo cha Mirza Ghulam Ahmad sahib siyo cha kuacha kupata funzo ndani yake. Mtu ambaye husababisha mapinduzi duniani ya kidini au kiakili huwa hazaliwi mara kwa mara daima, (ni nadra sana kuzaliwa duniani) na wanapokuja basi hufika na huonyesha mapinduzi duniani. Upeo huu wa juu wa Mirza sahib ingawa umesababisha tofauti kubwa kutokana na kutofautiana sana kiitikadi kwa madai yake lakini pamoja na tofauti hizi kwa Waislam hasa Waislam wasomi na wenye mawazo yenye mwanga wanahisi kuwa mtu wao mkubwa sana ametengana nao. Na mapambano makali aliyoyaongoza kwa ushujaa mkubwa dhidi ya wapinzani wa dini ya Kiislam yaliyoambatana – husiana na dhati yake yamefikia mwisho. Hasa ukizingatia kuwa yeye alijitambulisha jemedari mshindi wa mapambano dhidi ya wapinzani wa Islam, ndiyo yanayotulazimisha tuikiri hali hiyo waziwazi, maandishi ya Bw. Mirza sahib aliyoyadhihirisha dhidi ya Maariya na dhidi ya Wakristo yanafahamika mno katika jamii na yamekwisha kubalika. Kutokana na ubora na adhama ya maandishi hayo, leo ambapo yeye amekwisha kamilisha kazi zake sisi tunalazimika kukiri kuwa hatuna tumaini kuwa katika ulimwengu wa kidini mtu wa shani na hadhi hii atazaliwa katika ardhi ya India huko baadae."

Gazeti moja lisilokuwa la Waahmadiyya lilikuwa linaitwa "TAHDHIIBUN NISWAN". Mhariri wake anaandika kuwa; "Marehemu Mirza sahib alikuwa mtu mtawa sana, na alikuwa na nguvu ya utawa kiasi hiki kwamba hata moyo mgumu kweli kweli yeye alikuwa anaulainisha. Alikuwa mjuzi wa habari nyingi, mwenye hima na azma ya hali ya juu sana, yeye alikuwa mfano mzuri kwa maisha matakatifu. Sisi hatuwezi kumwamini kidini kuwa yu Masihi Mauud, lakini miongozo yake kwa ajili ya mioyo iliyokufa yeye kweli alikuwa na sifa za kimasihi kwao" .

Mhariri wa gazeti la Kiariya la mjini Lahore; "ARIYAPATAR KA" Anaandika kuwa; "Kwa kawaida Uislam unaojulikana kupatikana kwa Waislam wengine, mawazo ya Uislam ya Mirza sahib yalikuwa yamepanuka na yana vumilika zaidi kuliko ya wengine. Mahusiano ya Mirza sahib na waumini wa Kiariya kamwe hayakuwahi kuwa ya kirafiki, na tunapoidunusu historia iliyopita ya Ariya Samaj tunakuta ndani ya mioyo yetu uwepo wake (Hadhrat Masihi Mauud) unazalisha jazba na joto" .

Gazeti la Ariya – Lahore "INDAR" likaandika kuwa; "Katika sifa moja Mirza sahib alishabihiana sana na Bw. Mtume Muhammad saw, na sifa hiyo ilikuwa ni kuliendesha kusudio alilolidhamiria. Sisi tunafurahi kuona kuwa yeye mpaka mwisho wa uhai wake aliligangamalia kusudio hilo licha ya pingamizi maelfu kwa maelfu, lakini hakutikisika hata kidogo" .

Gazeti moja la Kiingereza litowela kutoka Allah Abad "Pioneer" likaandika hivi kuwa; "Miongoni mwa Manabii wazamani wa Kiisraili kama mmoja arudi leo na afanye mahubiri, basi katika zama hizi za karne ya ishirini hataonekana mwenye kufaa zaidi tofauti na alivyokuwa Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian. Mirza sahib hakuwahi kamwe kuwa na shaka juu ya madai yake na kwa ukweli kamili na uaminifu alikuwa na yakini juu ya jambo hili kuwa yeye anateremshiwa ufunuo wa Kiungu na kwamba yeye alikuwa amepewa nguvu zisizokuwa za kawaida. Safari moja yeye (Mirza sahib) alimwita kwenye mashindano Bishop Weldon wa Culcutta India washindane katika kuonyesha alama, nae Mirza sahib alikuwa tayari kwa jambo hili kuwa kulingana na hali ya zama hizi, Bw. Bishop vyovyote ilivyo ajiridhishe kuwa katika kuonesha nishani – alama hiyo – hizo, aina yoyote ya udanganyifu isitumike. Watu wale waliozalisha harakati katika ulimwengu wa dini ndani ya hali zao kwa kulinganishwa na Lord Bishop wa Uingereza wanafanana sana na Mirza Ghulam Ahmad, kwa vyovyote vile, Nabii wa Qadian alikuwa ni miongoni mwa watu wale ambao hawatokei mara kwa mara duniani."

Bw. Walter M.A Katibu wa All India Christian Association katika kitabu chake cha Kiingereza 'Ahmadiyya Movement' anaandika kuwa; "Jambo hili linathibitika kwa kila hali kuwa Mirza sahib katika desturi zake alikuwa mtu wa kawaida na mwenye jazba za ukarimu, khulka zake za kishujaa alizozionyesha alipokabiliana na upinzani mkali wenye madhara, kwa kweli ni wa kusifiwa. Ni mtu m wenye mvuto wa kisumaku na khulka njema tu ndiye anayeweza kuteka uhusiano wa kirafiki na uaminifu wa watu ambapo miongoni mwao kwa uchache watu wawili wamejitolea maisha yao wakafa huko Afghanistan kwa kutetea imani n a itikadi zao lakini hawakutengana na Mirza sahib. Mimi nimewahoji baadhi ya Waahmadiyya wa zamani sababu za wao kujiunga na Uahmadiyya, wengi miongoni mwao wakataja kuwa sababu kubwa ni athari zake mwenyewe zenye mvuto wa kisumaku wenye jazba ya hali ya juu. Mwaka 1916 nilitembelea Qadian (ilhali miaka minane iliishapita tangu Hadhrat Masihi Mauud afariki) nikakuta Jamaat yenye waumini waliojaa jazba ya kweli ya dini ambapo siku hizi nchini India imani hiyo imetoweka ndani ya Waislam wa kawaida. Baada ya kwenda Qadian mtu anaweza kuelewa kuwa roho ya ile imani ya Muislam anayoitafuta bila kuipata ndani ya Muislam wa kawaida imani na jazba hiyo vimejaa ndani ya Jamaat ya (Hadhrat) Ahmad kwa wingi" Ewe Masihi mtawa wa Allah! Salaam kemkem na rehema za Mungu ziwe juu yako, kuwa wewe kwa mifano yako mizuri na mafundisho yako matakatifu umepanda mbegu duniani ambayo ni mbegu ya kuleta mapinduzi makubwa sana ya kiroho ambayo pamoja nayo yamekadiriwa pia mapinduzi ya kimaada. Mbegu hii sasa itakuwa, itakomaa, itapevuka, itaenea kote na itaishinda miti ya bustani zote duniani, na hakuna yeyote wa kuizuia. (Ee Mola wetu msalie na mteremshie rehema yeye na juu ya Mtukufu Muhammad (saw) uwabarikie na uwaweke chini ya ulinzi wako).

Ndugu wanajamaati, jihadi hii ya kuitetea Islam kwa kutumia kalamu hadi leo inaendelea na kwa fadhila na msaada wa Allah tunaikuta jumuiya katika kuitetea islam ikiwa imesimama mbele na kwenye safu ya kwanza. Leo duniani kote endapo kuna jumuiya ambayo inawakilisha islam na kujitahidi mno katika kupigana jihadi dhidi ya wapinzani wake wote kwa kutumia silaha za kalamu basi ni Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tu.

Wassalaam.

Bustani ya Washairi

PERA

Ewe Mola Muadhama, nuru iliyo mwanana
Sikia yangu kalama, mja nisiye kifana
Umetuumba insar, kwa umbo bora sana
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Dunia ipana sana, na matunda mengi sana
Tena yasiyo kifana, umewapa insane
Hatana bwana zidana, wa kule mbali boswana
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Mwaka juzi na wa jana, niliongea majona
Amenihusia sana, kuiba yashindikana
Kakataza maulana, kitabu usomesana
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Hapo nikashikat ama, maswali yakinisuta
Nikaazimu kulima, nambegu kuitafuta
Nikaenda na kahama, kwa gharama za matata
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Makondeni na milima, shamba nikalitafuta
Nikaelezwa kwa juma, niende kumtafuta
Ndiye yeye mkulima, alima sana ufuta
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Ewe mwingi wa rehema, shamba ninalitafuta
Nijalie lilo jema, nisipande tu ufuta
Kila nafaka kulima, nazile zenye mafuta
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Beti saba zimefika, naweka chini kalamu
Na kitini nainuka, muda umenilazimu
Bongoni yamenitoka, kuyashika silazimu
Lipo wapi langu pera, kutoka kuleAdeni?

Al-Ustadhi Ally S. Magana (The new big boss)
Mkuyuni – Morogoro.

JANI

Bisimillahi auni, sifaye wetu Manani
Kalami ya mkononi, andikayalo moyoni
Dunia ni kitu gani, kwani mingi mitihani
Binadamu si chochote, ifikapo sina budi

Wapiti wenginjiani, nifanyejemiyejani
Uwezowanguniduni, hoi hoitaabani
Sipungukimidomoni, hatawalomajinuni
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Lo wengihunilaani, ningalihaikwanini?
Sinatena mi thamani, nafasisinamtini
Siogopikwendachini, ilakunamakatuni
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Uwapi ewe Manani, uniwekerehemani
Mimi wakoinsani, niongoze m iyeduni
Yupitenamdhamini, usiniachenjiani
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Japo macho hayaoni, kutembeanatamani
Akiliyangumakini, sinanguvumiguuni
Thabbitiaqdamani, imenaswamatopeni
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Kosalangumiyenini, kulasikutujuani
Nayetawimkoloni, kaniwekaduniani
Leo hiihanitamani, sinafaidamachoni
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Naliamwenzenujani, pakushikasipaoni
Rafikipiamtini, hatashorwesimuoni
Kiliochangumwishoi, Mwenyezinipeauni
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Kaditamakituoni, sitakifikamjini
Kwaniwenginiwahuni, name badoujingani
Simbalikwetunyumbani, tafikahatajioni
Binadamusichochote, ifikaposinabudi

Al-Ustadhi Ally S. Magana (The new big boss)
Mkuyuni – Morogoro

KIBURI SI MUUNGWANA

Kwa jinaleMsifika, nashikayangukalamu
Jinale wetu Rabuka, sifaze zilo karamu
Mtukufu salimika, mitihani nijukumu
Kiburi kwa mwanadamu, si kitu chema kiburi

Kitabunikuzipika, kuzipanguahesabu
Si kazi ya urimboka, Rabanandiyehabibu
Machoziyakumwagika, waungwanasiajabu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Ikiwaumeumbika, kwauzuriulotimu
Au umetajirika, pesanyingitasilimu
Kiburiukajivika, vazilenyeuhasimu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Majukumusifanaka, ndiyokaziyeKarimu
Ukawangejifunika, kuwasibuwanadamu
Kwa kuzionafanaka, molaalokukirimu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Molamwenyemadaraka, n diyemwenyekurehemu
Humpaanayetaka, jamii ya wanadamu
Majukumusifanaka, kufanyizana karamu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Waringanahekaheka, wenzakokuwashutumu
Kwanza ziondoe taka, nduguzokuwahasimu!
Usiipigemipaka, ukakushikawazimu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Kiburimbayamkeka, kukalianiharamu
Yapendezakukumbuka, msemowenyekudumu
Mpandangazihushuka, alachokikawasumu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Na mwanadamuyataka, bongo lakokulitimu
Wazeewalotamka, manenoyalomuhimu
Kulonamahuinuka, lainihuwakigumu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Wauminitwakutaka, jaliawetuimamu
Zetu jihasafishika, ng'arisha zetu nidhamu
Ng'ambotwatakakufika, tuepushemasanamu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Kaditamanimefika, nazikomeshanudhumu
Yanatoshayalofika, kiburinimuhasimu
Muungwanaatashika, asoshikasilazimu
Kiburikwamwanadamu, sikituchemakiburi

Al-Ustadhi Ally S. Magana (The new big boss)
Mkuyuni – Morogoro

ENYI MASHEHE MWATISHA

Enyi mashehe wa sasa, nawaapia Manani
Kuwa kiroho mwatisha, enyi mlo makundini
Mlo makundini hasa, hayo yote eleweni
Yalosemwa fawahisha, kwenye Islamu dini
Yote ni ya kupotosha, yatia watu motoni
Enyi mashehe mwatisha, mlo humo makundini

Muwabaya wa kutosha, sababu nawambieni
Nabii aliyefika, muhuisha upya dini
Ya Mola ilotoweka, ilohama duniani
Ipate rejea upya, Izishinde zote dini
Ninyi mnamkanusha, hamtaki muamini,
Na uongo mnazusha, mwingi wa kumfitini.

Kisha aloyarejesha, mnayo yaona nanyi
Kwenu yana muafaka, mwayatumia juweni
Na kisha mwajionesha kuwa nanyi ni wasomi
Mno mwajifaharisha, eti mnajua dini
Mwajifanya kama hasa, zama hizi duniani
Upya mnaifundisha, dini ya Mola Manani.

Kumbe nawafahamisha, kiroho muujingani
Mumo ujingani hasa, mkubwa uso kifani
Sababu nawajulisha, huyo muhisha dini
Kafika mwamkanusha, alotumwa na Manani
Mwamkana katakata, hamtaki muamini
Hivyo wazi mwaonesha, kuwa mko ujingani.

Wazi wazi mwaonesha, kiroho muujingani
Elimu ya dini hasa, hamnayo asilani
Upya iliyorejeshwa hiyo ya Mola Manani
Ingawa mwabakabaka, mwaidokoa na nyinyi
Bali hamjaipata, halisi wake undani
Katu hamjaigusa, na sababu yake nini?

Ingawa mwabakabaka, elimu hiyo ya dini
Bali hamjaipata, bado mmo ujingani
Na sababu nini hasa, nawaeleza juweni
Bado hamwetakasika, nanyi mmo ujingani
Muwapinzani hakika, mwapingana na Manani
Nabii aliyefika, hamtaki muamini.

Nabii aliyefika, huyo mrejesha dini
Mwamkana katakata, na pia mwamlaani
Na watu mwawapotosha, wakose kumbaini,
Nao mwawasababisha, kiroho wasimwamini
Enyi mashehe mwatisha, mulo humo makundini
Muwabaya wa kutosha, kimbingu nawambieni.

Kuwa muwabaya hasa, tena mumo hasarani
Maana nawafahamisha, mumo kwenye kundi gani
La Summun fawahisha, bukum, Umyun
Hivyo nawaelewesha, muelewe si utani
Bilisi kawafumbata, mumo mwake mikononi
Haki mkielimishwa, ni shida kuiamini

Kila mkielimishwa, mkielezwa undani
Kuwa huyo alofika, ni nabii wa Manani
Dini kaja kurejesha, Ya Mola ilotuhuni
Mwamkana katakata, na sabbau hasa nini?
Mnasema umeisha utume wake Manani
Hauji tena maisha ushafikia mwishoni

Kila mkifahamishwa, ukweli muubaini
Huyo alietufika, si muongo asilani
Ni nabii hana jipya, kaja kuhuisha dini
Ile ile ilo achwa, kwa umma ikatuhuni
Bali huwa mwazidisha, viburi mwasema nini?
Utume umeshaisha, huyo ni mtume gani?

Kumbe nawafahamisha, elimu zenu juweni
Mtumiazo hakika, ni batili za motoni
Zilizosemwa za vichwa, watu walizozibuni
Hizo mlizorithishwa, mno mnozithamini
Ndizo zawasababisha, mbakie ujingani
Msijuwe uloisha, hasa ni utume gani?

Elimu zenu za vichwa, mulorithishwa na ninyi
Motoni zawapeleka, kisa na sababu gani?
Hamjui uliosha, hasa ni utume gani
Nabii wa Mola hasa, zama hizi eleweni
Huyo aliyetufika, kuturejeshea dini
Mwabaki kumkanusha, kina mkimfitini

Hamjui uloisha, hasa ni utume gani?
Elimu hizo za vichwa, wallahi zawafitini
Motoni zawapeleka, kisa na sababu nini?
Dhahiri mwamkanusha, Mnamuasi Manani
Kisa unabii hasa, uliofika mwishoni

Kisa Unabii hasa, uliofika mwishoni
Fasiri mwaipotosha, kwa elimu za vichwani
Wazi zilizotamkwa, si njema ni za kubuni
Hivyo mwaubadilisha utume wake Manani
Mwishoni uliofika, mwaupotosha undani
Haki mwaibadilisha, mwaisaliti na nyinyi

Nanyi mwaibadilisha, haki ya Mola Manani
Wazi nawaelewesha, mwaitia batilini
Mfano wenu halisa, ni ule wa Makuhani
Wao na nyinyi hakika, mmefanana juweni
Kiroho nanyi mwatisha, kama wao sikieni
Nanyi muwabaya tosha, kimbingu jieleweni.

Kimbingu nawajulisha, muwabaya pia nanyi
Mfano wenu halisa, ni ule wa Makuhani
Masihi wenu hakika, keshafika duniani
Kwa hamu kubwa kabisa, mulomsubiri nanyi
Lakini mwamkanusha, kina mkimfitini
Na watu mwawapotosha, nao wasimuamini.

Kimbingu jama mwatisha, mashehe wanazuoni
Wa makundi ya kuzusha, yalosemwa ya motoni
Ambao ndio hakika, Mlosemwa eleweni
Ni shida kusalimika, atakayewaamini
Motoni atapelekwa, yeye pamoja na ninyi
Muhammad katamka, hayo katia saini.

Mwatisha jama mwatisha, Mashehe nawambieni
Wa makundi ya kuzusha, ya elimu za vichwani
Motoni mwawapeleka, nawapia na Manani
Wasiotaka zinduka, hao wenu waumini
Mwisho wake watajuta, majuto huja mwishoni.

Wajijue vya kutosha hao wenu waumini
Ambao mwawapotosha, huyo muhisha dini
Wamkane katakata, na wao wasimwamini
Mwisho wake watajuta, wajue huo undani
Maana mtawakuta, mbele ya Mola Manani
Sababu yanawafika, mahubiri wayalaani.

Wajijue fawahisha, hao wenu waumini
Iwapo hawazinduka, wanayopewa maoni
Basi mwisho watajuta, mbele ya Mola Manani
Maana mtawakuta, muwambie kitu gani?
Mahubiri walipata, akili zao vichwani
Kutumia hawetaka, haki wakaibaini.

Bimkubwa Kombo, Zanzibar

Nyota ya Kusini Yazimika

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Lakabu niliyoisikia mara kwa mara mwaka 1965 ikitajwa hapa Masjid Salaam ni 'Nyota ya Kusini'. Wakiwa wanaashiria Maulana Sheikh Fadhlillahi Bashiri Mbashiri ambaye amefanya kazi kubwa ya kusambaza nuru ya Ahmadiyya kusini mwa taifa hili. Nyota hiyo ya kusini imezimika (Innalillahi wa inna ilaihi Rajiuun - Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea) lakini imeacha athari kubwa katika nyoyo zetu.

Sheikh Fadhillahi Bashiri ni miongoni mwa wabashiri wa Mwanzo mwanzo kutumwa Afrika ya Mashariki. Na nchi ambayo alifanyia kazi sana ni Tanzania ingawaje aliwahi kutoa huduma yake katika nchi ya Mauritius.

Sheikh Fadhillahi Bashiri alikuwa na mapenzi makubwa na watu aliokuwa amekuja kuwapa habari za kufika kwa Masihi wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Mtindo wake wa mahubiri ulikuwa ni wa kwenda nyumba moja hadi nyingine akieleza kwa upole na mapenzi juu ya ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Na kabla hajazungumza aliomba rukhsa na aliyekataa aliondoka. Taratibu habari zilianza kuenea ya kwamba Lindi imevamiwa na Qadian. Wasiwasi ilitanda na Masheikh wakakutana ili kutatua tatizo hilo. Ilikubaliwa ya kwamba Sheikh Fadhillahi Bashiri aitwe na aweze kueleza kinaga ubaga itikadi yake.

Mkutano mkubwa uliitwa mjini Lindi na Masheikh ili wamuulize kadamnasi Sheikh Fadhillahi Bashiri itikadi yake ambayo sawa na Masheikh hao inamuweka mtu nje ya Islam. Ulikuwa ni mkutano mkubwa uliohudhuriwa na watu wengi wenye jazba na hasira. Sheikh Yusuf (suni) kwa niaba ya Masheikh wa Lindi alisimama na kumuuliza Sheikh Fadhillahi Bashiri Imani yake ilikuwa ni nini? Sheikh Fadhillahi Bashiri huku akitabasamu alisimama na kutoa Assalaam Alaikum warahmatullah wabarakatuh kwa umati uliokuwa umehudhuria. Ingawaje baadhi hawakujibu. Kwa sauti ya mvuto lakini iliyowakera Masheikh Sheikh Fadhillahi Bashiri alisema; "Nashukuru sana Mwenyezi Mungu Aliyeniwezesha kufika nchi hii. Namshukuru pia kwamba Alhamdulillah nimewakuta ndugu zangu Waislam. Ni neema kubwa ilioje. Nimeulizwa 'Itikadi yangu ni ipi? Swali zuri na bila shaka litapata jibu zuri pia. Ndugu zangu Waislam itikadi yangu ni kuwa; Hakuna Apasaye kuabudiwa Isipokuwa Allah na Mtume Muhammad (saw) ni Mjumbe Wake. Alipomaliza tu kusema hivyo sauti za hasira zilisikika pande zote. 'Kafiri huyo, kafiri mkubwa huyo!! Mzee Karuma Isa aliyekuwa katika mkutano huo alipigwa na bumbuwazi kubwa. Huyu mtu katoa shahada na bado wanasema huyu ni kafiri?! Damu ilimchemka Mzee Karuma Isa akazidi kutetemeka jasho lililowanisha shati lake. Sauti za hasira zikaanza kusikika; 'apigwe kweli kweli huyo kafiri mkubwa!! Atatuharibia Uislam wetu!' bila kufahamu anachofanya Karuma Isa alikuwa karibu na meza kwa haraka alivunja meza ile na kwa kuchukua mguu wa meza akatangaza; 'Nione mtu amguse mtu huyu!' watu walimtishia Karuma Isa kwa kusema; 'Tutawachanyata nyote'. Lakini Karuma Isa hakutetemeka hata kidogo. Alishagundua ya kwamba akimwacha angeweza kuumizwa vibaya sana hivyo akajitolea kumlinda. Na akamwambia; 'Sheikh usiwe na wasiwasi, taratibu waliondoka eneo la tukio huku umati wa watu ukiwa bado unawafuata na huku wamefura. Karuma Isa alipita kwa DC kwani kazi yake yeye alikuwa ni mpishi wa DC. Dc alitoka nje na kumuona Karuma Isa amebadilika sura na akamuuliza; 'Kuna nini Karuma Isa'! Karuma Isa akamueleza yote yaliyotokea. Hivyo akamruhusu Karuma Isa amsindikize Sheikh hadi nyumba aliyokuwa amepanga. Hapo kwa utulivu akapata fursa ya kumuuliza Imani ya Ahmadiyya na jioni akaweza kukutana na baadhi ya Wanajumuiyya ya Lindi ambao tayari walikwisha jiunga na Jumuiyya akiwemo Ahmad Ismaili Mpukutile, Mwisheweji, Ahmad Mataka Busra, na kutoka si ku hiyo Karuma Isa akawa katika jeshi la Mahadi na alipigana kiume katika kulinda mafundisho ya Masihi Aliyeahidiwa.



Maulana Fazl Ilaahi Sahib, akiwa amesaidiwa na mtoa huduma ya ubebaji wakati wa Jalsa Salana 2007 Qadian, India.

Ahmadiyya katika Lindi ikapata nguvu kutokana na kujiunga na Karuma Isa ambaye alikuwa anafahamika kwa ngumi na mieleka. Na watu Lindi wakasema basi kama Karuma Isa ameingia basi Ahmadiyya hakuwa wa kuwagusa tena.

Kabla ya kujiunga Karuma Isa katika Ahmadiyya kundi dogo lililokuwa limejiunga na Jamaat lilinyanyaswa. Kwa mfano hawakuruhusiwa kununua vitu sokoni, kuchota maji kwenye visima, kunyang'anywa wake, lakini yote hayo yalipungua pindi alipojiunga Karuma Isa.

Siku moja katika harakati za mahubiri Sheikh Fadhillahi Bashiri alivamiwa na adui aliyebeba kisu na aliyekuwa na nia mbaya. Mungu bariki alitokea kwa mara ya pili Bwana Karuma Isa bila ya woga wowote alishika kisu kile alichokuwa anataka kumchoma nacho Sheikh Fadhillahi Bashiri na alikuwa amekama kwenye makali lakini hakujali kuumia hadi akafaulu kumnusuru Sheikh Fadhillahi Bashiri.

Historia ya Jamaat ya Tanzania inaeleza sana juu ya kimbunga cha Lindi kilichotokea mwaka 1952. Matokeo mengi yanayotokea ikiwa tunafanya utafiti wa kina tunaweza kupata chimbuko lake. Kimbunga cha Lindi kilitikisa mji wa Lindi na magazeti ya enzi hizo yalieleza juu ya tukio hilo. Sababu zinaweza kuelezwa lakini bila shaka Jumuiyya ya Ahmadiyya ina sababu nzuri Zaidi za kueleza juu ya tukio hilo. Ni kama tukio lile lile la Tanzania kuwa kisima cha Amani. Lakini watu hawaelewi kwamba siri kubwa ya Amani ya nchi yetu ni maombi ya mara kwa mara yaliyokuwa yanafanywa na Khalifatul Masih –II (Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad ra) hadi kufikia hatua ya kusema 'Tanzania ni nchi yetu'. Kwa kutumia kigezo kama hicho tunaweza kutazama kimbunga cha Lindi cha mwaka 1952.

Sheikh Fadhillahi Bashiri kama tulivyokwisha ona aliendelea kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (as). Sheikh Badi –kiongozi maarufu wa kisuni mjini Lindi hakufurahishwa na kazi ya Sheikh Fadhillahi Bashiri. Yeye aliona ni njia ya kuwapoteza Waislam na kutia kitumbua chao mchanga. Hivyo sheikh Badi alimtaka Sheikh Fadhillahi Bashiri awe na mjadala nae. Mjadala huo ulichukua siku nyingi na siku zote ilidhihirika kuwa elimu ya Sheikh Badi ilikuwa ndogo. Silaha pekee aliyobaki nayo Sheikh Badi ilikuwa ni kuwaamuru wafuasi wake kuzomea. Kwa hiyo Sheikh Fadhillahi Bashiri akawa anazomewa. Kuzomewa huko kuliendelea na Sheikh Badi akitia pamba katika masikio yake. Akiwa amevumilia kiasi cha kutosha Sheikh Fadhillahi Bashiri alimwambia sheikh Badi; "Mwenyezi Mungu Atashuka hapa" kwa kebehi Sheikh Badi akasema; "Mwenyezi Mungu Ashuke ana miguu?". Kwa upole Sheikh Fadhillahi Bashiri alimwambia sheikh Badi; "Mwenyezi Mungu Atashuka kwa kudra yake". Kauli hiyo kutoka kwa Sheikh Fadhillahi Bashiri ilikuwa nzito. Aliwaomba wanajamaat wote waondoke mjini Lindi kwani kwa msaada wa Mwenyezi Mungu alikuwa na uhakika wa yale aliyokuwa anayasema.

Alipohakikisha Wanajumuiyya wakwishatoka mjini Lindi alifunga safari ya kuelekea Songea. Alilala siku moja mjini Songea kesho yake huko Lindi ikatokea zilzaalahaa ambalo masimulizi yake yanapatikana hadi hivi leo. Lilikuwa ni tufani, kilikuwa ni kimbunga, tetemeko utadhani kila

Endelea uk. 8

UJUMBE WA JALSA SALANA TANZANIA KUTOKA KWA HADHRAT KHALIFATUL MASIH WA TANO (ATBA)

Wapendwa Waahmadiyya wa Tanzania,

Assalaamu Alaikum Warahmatullaahi Wabarakaatuh.

Alhamdulillah kwamba Jalsa Salana ya Tanzania inafanyika. Jalsa hii ni sababu ya baraka kwa Muahmadiyya na inapaswa iwe hivyo. Kwa sababu kukusanyika katika mazingira fulani makhsus kwa ajili tu ya makusudio ya kidini, kwa ajili ya kumkumbuka Allah, kujumuika kwa ajili ya kupata ridhaa Zake na furaha Yake, kwa hakika hiyo ni njia ya kuzivuta fadhili za Allah, kama vile mpendwa wetu Mtume Muhammad s.a.w. alivyosema kwa uwazi kabisa kwamba mikutano inayofanywa kwa ajili ya kumkumbuka Allah husababisha watu wawe warithi wa fadhili za Allah. Huongoza kwenye Pepo Zake.

Mtume s.a.w. alisema: Enyi watu! Jitahidini kujilisha ndani ya bustani za Peponi. Maswahaba walipotaka ufafanuzi wa kauli hii kwamba Bustani za Peponi ni nini? Basi Mtume s.a.w. akasema kwamba vikao vya kumkumbuka Allah ndio bustani za Peponi. Kumbukeni kwamba Makusudio ya Jalsa Salana aliyoyabainisha Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. ni haya kwamba kwa ajili ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu, jitahidini kupiga hatua katika mapenzi ya Allah. Pigeni hatua katika Ucha Mungu. Elekeeni pia kwenye maombi na ibada na kuwe na mwelekeo kwenye utoaji wa haki za waja wa Allah.

Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliwaombea sana wale wenye kushiriki katika mikutano hii ya Jalsa Salana kwamba Allah Awalipe malipo makubwa sana wale wanaoshiriki kwenye Jalsa Salana na Awarehemu na Awarahisishie matatizo na wasiwasi wao na Awaondolee huzuni na majonzi yao. Kwa ajili ya kuwa mrithi wa kweli wa maombi haya, yapaswa kwamba kila Muahmadiyya ayazingatie makusudio ya Jalsa hizi na afanye juhudi kubwa kabisa ya kujibadili ndani mwake na kuwa mtu mwema. Aelekee kwenye kutubu na kuomba msamaha na huku akiwa ameinama mbele ya Allah, amuombe ghofira na msamaha. Allah Akujaalieni nyote uwezo wa haya na Akufanyeni warithi wa fadhili Zake.

Allah Amewafanyia Waahmadiyya hisani hii kwamba Ametupatia tena neema ya ukhalifa baada ya kumuamini Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. na Ametuunganisha na nidhamu hii ambayo kwayo kila mwanajumuiya anakuwa mara kwa mara anaelekezwa kwenye utii wa Allah na Mtume Wake. Utii ndilo jambo ambalo kwalo mafanikio hupatiana.

Yaani wale wenye kurithi neema za Allah, mafanikio na ushindi ni wa wale tu walio wenye kutii na mafanikio na maendeleo ya Jumuiya yameambatana na hali hii ya utii. Kila aliyefanya Baiat, awe mwanaume au mwanamke, hushika ahadi hii kwamba yeye ataitanguliza dini juu ya dunia na atadumu kujitahidi katika kuletesha maendeleo ya nidhamu ya Jumuiya.

Hivyo kila muahmadiyya anayejitahidi katika kukuza viwango vyake vya ibada, basi afanye pia juhudi ya kukuza viwango vyake vya utii kwa Khalifa wa zama, kwani kwa ajili ya kukubaliwa kwa ibada ni lazima kumtii Khalifa wa zama. Ndio sababu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema: Jitihada za ibada hazina umuhimu kama zilivyo za utii. Hivyo kila Muahmadiyya atalazimika kubeba shingoni mwake uzito wa utii kamili.

Allah Akupeni nyote uwezo wa kuyafahamu mambo haya na kuyatekeleza. Muwe wenye kufuata maagizo ya Qur'ani Tukufu na ya Mtume s.a.w. Muwe wenye kuitanguliza dini juu ya dunia. Muwe wenye kumuauni na kumsaidia Khalifa wa zama na Muwe wenye kuzikusanya fadhili za Allah, Amin.

Wassalaam, Mnyenyekevu

Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih 5

Nyota ya Kusini Yazimika

Kutoka uk. 7

kitu kinataka kukatika vipande vipande. Upepo ukaangusha miti, mji wote wa Lindi ulijikunyata na hakuna liyediriki kutoka nje. Barabara zilikuwa hazipitiki kwani zilikuwa zimefunikwa na miti. Waya za umeme zilikuwa zimetanda mahala pote. Hata ndege wa angani walikuwa kimya.

Ni wafungwa waliotumika kutumika mji wa Lindi katika hali yake. Walipita mjini kuondoa miti na kusafisha mji. Sheikh Fadhillahi Bashiri aliporudi mjini Lindi akakutana na Sheikh Badi na kumuuliza; "Sheikh Badi umemuona Mungu?". Sheikh Badi alikaukiwa mate. Akatweta kama farasi aliyetoka kwenye mashindano, alijiinamia chini kwa aibu.

Kama hujaongozwa kwa msaada wa Allah, miujiza inasaidia nini? Akina Abu Jahal waliona miujiza mingi, lakini sikio la kufa halisikii dawa. Ndugu wa Ahmadiyya kujiepusha na shari na sawa na suna ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) walienda zao kuishi mahali palipoitwa jangwani. Sheikh Fadhillahi Bashiri alikuwa mlezi wa wana. Alipenda sana kuwatembelea kondoo wake ili kuwaepusha kutoliwa na mbwa mwitu. Katika moja ya safari za kuwaona wa Ahmadiyya waliokuwa jangwani alikutana na Simba. Na simba huyo alimsindikiza hadi nyumba za wa Ahmadiyya na akarudi.

Maadui hawakuridhika na utulivu waliokuwa wameupata Waahmadiyya huko jangwani. Siku moja watu watatu Saidi Abdallah Waga, Kalidode na Kachingwa wakiwa kwenye baiskeli mpya walifunga safari hadi jangwani walikokuwa na dhamira ya kuanzisha fujo na bughudha. Jitihada zao hizo ziligonga mwamba. Saidi Abdallah Waga alishika ndevu za Sheikh Fadhillahi Bashiri na kuzivuta. Wafuasi wa Sheikh Fadhillahi Bashiri walihamaki lakini Sheikh Fadhillahi Bashiri kwa sauti ya upole alisema; "Muache hajui alifanyalo". Miaka michache baadae bwana Saidi Abdallah Waga alijiunga na Waahmadiyya ni kisa cha kusisimua.

Bwnaa Saidi Abdallah Waga alishindana na wenzie juu ya kuchinja. Waga alisema njia nzuri ya kuchinja ni kukata mishipa ya fahamu ya kuku na kubakisha ngozi. Wenzie walisisitiza kukata moja kwa moja kichwa chote. Ubishi huo ulipoendelea wakaanza kusema; "Vipi Bwana Waga? Hatukuelewi! Mbona unaonekana kuwa kule kule". "Kule kule wapi?" aliuliza Saidi Abdallah Waga. Masingizio hayo yalikuwa yanaashiria Jumuiyya ya Ahmadiyya. Jambo hilo la dhana lilimuudhi sana bw. Saidi Abdallah Waga na akaenda moja kwa moja kwa Ahmad Ismaili Mpukutile na akamuuliza maswali machache na akajiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya. Na aliendelea kuwa Mwanajumuiyya hadi kifo chake.

Kama walivyokuwa Masheikh waliokuja zama za mwanzo, Sheikh Fadhillahi Bashiri alikuwa na umahiri wa kutumia kalamu. Kwa kutumia kalamu alijenga hoja na kufanya maandishi yake yawe na utamu wa ajabu. Wakati akiwa Afrika Mashariki Sheikh Fadhillahi Bashiri aliandika Makala nyingi katika gazeti la Mapenzi ya Mungu. Licha ya Makala aliandika vitabu vyenye sifa ya kuwa dhifa ya kisomi. Kitabu chake; 'Al-Kawl Swaalih' kinapatikana katika lugha mbili za Kiarabu na Kifaransa. Hoja zilizojengwa zinathibitisha ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Ni hoja zinazoambatana na ushahidi. Ukimaliza kukisoma unabaki na njia mbili; kufanya ukaramsi wa kitoto na kujaribu kuziba nuru ya jua kwa kiganja au kufanya haraka na kumpokea Masihi Aliyeahidiwa (as). Kitabu chake cha pili kimo katika lugha ya Kifaransa; 'La Moite Glorious de Jesus Christ' ambacho maana yake ni "Kifo kitukufu cha Yesu Kristo". Ukimaliza kitabu hicho unakumbuka shairi la Sheikh Kaluta Amri Abedi; Nabii Isa afile, poleni bwana Padiri. Kama amefariki Mtukufu Mtume Muhammad (saw) nani anaweza kuepuka kikombe hiki?

Jambo la kufurahisha ni kwamba wale wote waliojiunga na Jumuiyya ya Ahmadiyya kwa mkono wa Sheikh Fadhillahi Bashiri walielewa vilivyo mafundisho yaliyotolewa na Masihi Aliyeahidiwa (as). Uthibitisho wa hayo yamo katika barua waliyomuandikia DC tarehe 15/10/1950 ambayo tunatoa nakala yake.



Waahmadyya Waislamu Wa Mingoyo na Mtama tarehe 15.10.1950

D.C.
Lindi.

Bwana uliyeheshimika!

Tunakusarifu kwa adabu nyingi na upole sana ya kuwa sisi tulikuwa waislamu hamna ya waislamu wa taifa zinginę hatukujua sheria ya Kiislamu iliyosafi na haki. Mwaka juzi alifika sheikh mmoja aitwae Sh. Fazal Ilahi Bashir katika inchi hii yetu tumempokea na tumesikia mafundisho yake, na maeleze yake . Tmemona mkwelik katika dini yake tumefuata.

Sisi ni waislamu Waahmadyya, tumemaini Syedina Mirza Ghulam Ahmad ndiye Mjumbe wa Mungu aliyeahidiwa na aliyepelekwa na Mungu kwa bin Adamu kufundisha na kueneza neno Lake(LA ILAHA ILLALLAHO MOHAMMAD UR RASULULLAHE) katika zama hizi. Sisi kwa kheyari yetu tumeingia katika Jamaa Ahmadyya, ndiye kheyari ya kila mtu kufuata dini ye yote atakaye.

1. Wasio Waahmadyya wamekasirika, na wameanza kujaribu kuturudisha kwao ,wakaanza kutubughudhi bure pasipokuwa na sheria. Walipoona haturudi wakaanza kututukana na kutusemea njiani na barabarani,na nyumbani mwetu pia kwa matukano machafu-na-matusi mabaya.-Sheikh wetu mwenyewe amestahamili na ametunasihi tusi-wajibu watacheka wenyewe na watacha lakini yeye hakujua taabu yetu. Kwa muda mrefu tumeweza kustahamili.

2. Waislamu hawa walipoona matusi yao na matukano yao hayafai, na hawapati makusudio yao kuturudisha katika kundi lao, wameambiwa na Sheikh Mohammad bin Yusuf wayanganye wake zetu bila sheria na ushahidi wa dini ya Kiislamu, hali yeye ni sheikh wa dini ya Kiislamu kama anajidai mwenyewe.

Bwe Bwana Mfalme wetu tulipoona mambo haya yanazidi kila siku mapia mapia, na yanatushinda nguvu yetu ya kustahamili na kwa hakika tumeshindwa kusubiri taabu hizi na adhabu hii, maana sisi Waafrika waskini wa Mungu hatuwezi kuka kubali khasara za wanawake ndio mali yetu na raha zetu.Tumefika kwa serkali kwa huzuni mno na tumeubisha mlango wake mara kwa mara.

Waahmadyya wanafuata amri hii ya Mungu"atiini Mungu na Mtume

Sheikh Fadhillahi Bashiri ameitumia Islam Afrika Masharikina Mauritius. Kazi hiyo ameifanya kwa mapenzi makubwa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu apokee jitihada yake hiyo.

Haiba ya Mfalme Suleiman a.s.

Na Mwalimu Abdullah Hamisi Mbanga, Rufiji



Al-Masjid al-Aqsā, Jerusalem, moja ya majengo makongwe yenye kuvutia duniani, likiwakilisha utaalamu wa usanifu majengo ulivyofikia kiwango kikubwa wakati wa Nabii Suleiman a.s.

Hadhrat Suleiman (as) ndiye Nabii anayetajwa kuwa maarufu Zaidi katika wana wa Israeli baada ya Musa (as). Suleiman pia anatajwa kuwa miongoni mwa wafalme wenye nguvu waliopata kutokea duniani.

Qur'an Tukufu inadokeza kwamba Suleiman alikuwa ni mtu aliyejaaliwa vipawa vingi vya hekima na utambuzi. (27:16). Kutokana na vipawa alivyojaliwa na pia umahiri na uadilifu aliouonyesha katika utawala wake, Suleiman (as) ameendelea kuenziwa sio na Waisrael tu, bali wanahistoria wengi wanamhesabu kuwa ni mtu wa kupigiwa mfano katika masuala ya utawala, uadilifu na ucha Mungu.

Kutokana na wema aliokuwa nao, Suleiman (as) alitokea kuwa mtu mwenye haiba kubwa katika zama zake. Wafalme, wanazuoni na hata raia wa kawaida katika enzi hizo, walimhesabu Suleiman (as) kuwa ni mtu aliyekuwa zaidi ya binadamu wa kawaida.

Katika kumuenzi Hadhrat Suleiman (as) riwaya nyingi ziliandikwa juu ya sifa zake. Hekaya kuhusu vipawa na uhodari wa Suleiman katika medani mbalimbali ziliendelea kuenezwa duniani kwa njia ya simulizi hata baada ya kifo chake.

Jambo la kusikitisha ni hili ya kwamba hekaya nyingi kumhusu Suleiman na maisha yake zilitiwa chumvi na wasimulizi – pengine kwa ajili ya kumpamba – hata ikapelekea kuibuka kwa taswira tofauti kabisa juu ya Suleiman na vipawa vyake. Pengine kutokana na ufahamu finyu juu ya baadhi ya aya za Qur'an Tukufu, hata baadhi ya wanazuoni wa Kiislam wamejikuta wakizikumbatia baadhi ya dhana potofu juu ya Suleiman na kuzihubiri kwa karne kadhaa katika vizimba vya Misikiti, Mikutano ya hadhara na hata kwenye madarasa mbalimbali. Hali hii ikapelekea Waislam wengi kuingiwana Imani kuwa Suleiman huenda alikuwa mtu wa ajabu aliyekuwa na vipawa vilivyopindukia uwezo wa kawaida wa kibinadamu.

Makala hi iinakusudia kuangazia ukweli juu ya dhana na mitazamo mbalimbali inayozunguka haiba ya Suleiman na maisha yake.

UFALME WAKE

Suleiman alirithi Ufalme kutoka kwa baba yake, Daud (as) anayetambulika kuwa ndiye Muasisi wa dola ya Kiyahudi, shujaa mkuu wa Israeli na Mfalme mwenye nguvu na haiba kubwa. Daud (as) ndiye aliyeziunganisha koo zote za Kiisraeli kutoka Dani hadi Beersheba na kuasisi dola kubwa ambayo milki yake ilienea kutoka mto Furat (Euphrates) hadi mto Nile. Ushujaa wa Daud (as) ulidhihirika Zaidi alipowaongoza Waisraeli katika harakati za kutanua milki yao. Aliongoza na kushinda mapambano mengi makubwa ambayo baadhi yake yalionekana kuwa ni hatari hata kwa maisha yake mwenyewe. Hadi leo hii katika medani za siasa, Daud (as) anatajwa kuwa ndiye baba wa taifa la Israeli.

Baada ya kifo cha Daud (as), Suleiman alitawazwa kuwa Mfalme wa Israeli. Yeye alianzia pale alipoishia baba yake na kuendelea kuitanua zaidi dola hiyo ya Kizayuni. Historia inaonyesha kuwa dola hii ilifikia katika kilele cha ustawi wake katika enzi za Suleiman wakati huo milki ya dola ya Kizayuni ilitanuka hadi Kaskazini mwa Syria kwa upande wa Mashariki mwa bahari ya mediterrania na kuteremka hadi katika eneo la bahari nyekundu (Sham), Ufalme huo ulienea katika bara Arabu hadi katika ghuba ya Uajemi.

Ni wakati wa Suleiman (as) ndipo dola ya Israeli ilipopiga hatua kubwa katika Nyanja za elimu, uchumi, utamaduni na hata ulinzi. Miongoni mwa alama kubwa za maendeleo ya kitamaduni zilizoachwa na Suleiman ni Hekalu lake lililopo Jerusalem (Masjid Aqsa) ambalo baadaye lilifanywa kuwa kibla ya wana wa Israeli. Hekalu hilo linaheshimiwa hadi sasa na limo katika orodha ya UNESCO (Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na sayansi na Utamaduni) kama mojawapo ya urithi wa dunia.

LUGHA YA NDEGE

Moja ya mambo yanayotamkwa kama maajabu ya vipawa vya Suleiman ni madai ya kwamba alijua lugha za ndege na wanyama. Hili ni jambo lililohubiriwa kwa shangwe kubwa na viongozi wa dini katika vizimba mbalimbali vya mahubiri yao. Baadhi yao hudiriki kurejea hata simulizi iliyomo katika Hekaya za Abunuwasi (kisa cha mtu aliyesikia lugha ya wanyama) kuwa kama ushahidi wa madai yao wakiamini kuwa mtu huyo si mwingine ila ni Nabii Suleiman bin Daud (as).

Dhana hii bila shaka inatokana na uelewa waliokuwa nao juu ya aya ya Qur'an Tukufu inayosema kuwa Daud na Suleiman walifundishwa lugha ya ndege (27:17). Lakini ukweli ni huu ya kwamba katika aya hii neno 'MANTIQAT TAIR' (lugha ya ndege) hayamaanishi lugha kwa maana ya mazungumzo yanayofanywa kwa kinywa na ulimi tu. Hapa neno 'MATIQ' lina maana pana Zaidi. Asili ya neno hili ni NUTQ ambayo maana yake hasa humaanisha mawasiliano ya kimaongezi kwa namna yoyote iwayo na silazima kuwepo na matamshi. Kwa mujibu wa kamusi ya Mufradatur Raghibul Asfahaani neno MANTIQ humaanisha lugha yoyote inayoweza kutoa maana ya neno, iwe ya sauti, ishara, alama au maandishi.

Ifahamike ya kwamba kila kiumbe kina njia yake ya mawasiliano na mazungumzo. Neno 'kusema' katika lugha ya Kiarabu humaanisha ishara yoyote inayotumika na kiumbe husik akutoa taarifa juu ya jambo fulani. Badala ya kauli ya kinywa hali ya kitu pia huhesabiwa kuwa ndiyo kauli. Kuna usemi wa Kiarabu usemao; 'IMTALA'A ALHAUDHU WA QABLA QATNII' (Pipa lilijaa likasema imetosha) hapa haimaanishi kuwa pipa lilitamka, bali maji yakimwagika huwa habari imeshatambulika kuwa pipa limejaa.

Kama kuna uandishi uliotumia kwa uangalifu maneno ya lugha na maana zake basi bila shaka ni uandishi wa Qur'an Tukufu. Kwani Allah Anapozungumzia lugha za maneno ya kinywa na ulimi hatumii neno MANTIQ bali neno lililotumika juu ya lugha ya aina hiyo ni LISAN kama inavyoonekana katika sura 14:10 na 30:23. Lakini neno MANTIQ linahusishwa na lugha ambayo kila kiumbe bila kujali lina sauti au la linaweza kuzungumza. Ndani ya Qur'an Tukufu kunatajwa habari ya baadhi ya viungo vya watu kutoa ushahidi juu ya matendo ya mja. Na inafanyika hivyo kama uthibitisho ya kuwa Allah hukisemesha kila kitu na katika aya inayozungumzia jambo hili neno lililotumika ni ANTAQA ambalo lina asili moja na MANTIQ (41:22). Kwa hivyo haimaanishi kuwa ngozi zitaota vinywa zitamke la! Bali zipo njia za kuifanya ngozi iweze kutoa taarifa zinazohusu mwili husika.

MANTIQ AL TAIR KATIKA DUNIA YA LEO.

Nabii Daud na Suleiman kudai kuwa wamefundishwa lugha ya ndege, ilikuwa ni taarifa juu ya fani muhimu ya kielimu ambayo huenda haikuwapo duniani kabla yao. Ifahamike kuwa ndege na wanyama wanazo njia fulani za mawasiliano ambazo sirahisi kwa mwanadamu kuzitambua bila elimu maalum. Hali kadhalika zipo njia na kanuni ambazokwazo mwanadamu anaweza kuwasiliana na wanyama na ndege. Katika jamii za wafugaji aghalabu elimu ya aina hii japo kwa kiwango kidogo hutumika katika uongozaji wa mifugo. Wanyama pia huweza kutoa ishara mbalimbali juu ya hatari iliyokaribu na hivyo kumfanya mchungaji wao kuchukua tahadhari.

Hii inaonyesha kuwa, wakatiwa Suleiman yumkini ndio wakati ambapo wanyama na ndege walianza kutumika katika shughuli mbalimbali za kiserikali ikiwemo za ulinzi, upelelezi na hata usambazaji wa taarifa mbalimbali.

Huu ni utamaduni maarufu mno kwa sasa duniani. Katika nchi mbalimbali wanyama wamekuwa msaada mkubwa katika upeoezi na utafiti. Leo hii si jambo la kushangaza kuona mbwa, nguruwe, vyura, panya n.k walitumika katika majeshi ya ulinzi na usalama kwa ajili ya kubaini wahalifu, mihadarati, silaha na hata ufichuaji wa mabomu yaliyotegwa ardhini.

Kuna taarifa nyingi juu ya wanyama mbalimbali kutumika kutoa taarifa muhimu na hata kubashiri mambo fulani yanayotarajiwa kutokea. Wazee wa kijadi katika nchi walikuwa wanatumia mnyama fulani anayefanana na kenge (kaka kuona) ili kujua kama mwaka huo una masika au ukame. Wajerumani waliwahi kutumia pweza kubashiri matokeo ya kombe la dunia la kandanda. Haya ni machache tu katika mambo yanayoweza kuitwa lugha za wanyama.

Leo hii tuonapo maafisa wanyamapori wakiwa mahiri kujua tabia na mawasiliano ya wanyama isidhaniwe kuwa ni nguvu za giza bali ni elimu wanayojifunza vyuoni. Kwa vyovyote iwavyo elimu juu ya lugha ya ndege aliyofunzwa Nabii Suleiman, bila shaka kupitia ufunuo wa Allah ilikuwa ni muhimu mno kwa ajili ya maendeleo ya kijamii. Uwepo wa mitandao ya habari inayojihusisha na elimu juu ya ndege na wanyama pori unathibitisha ukweli huu. Bila shaka dunia inayo deni kubwa kwa Nabii Suleiman ambaye yeye na baba yake waliitambulisha na kuiendeleza elimu hii duniani wakiacha urithi bora kabisa wa kielimu kwa vizazi vingi vilivyofuata. Hivyo ni wajibu wetu kuendeleza elimu hii na kuitumia kwa faida mbalimbali za jamii yetu hapo ndipo tutakuwa tumefikia ufahamu wa kweli wa maana ya 'MANTIQ AL TAIR' (Lugha ya ndege) elimua mbayo Allah Alimtunukia Hadhrat Suleiman (as).

Muongozo juu ya Tabligh na Tarbiyyat

Kutoka uk. 12

hadi leo Huzur Aqdas ameendelea kutukumbusha kila mara na kwa kila jiha juu ya wajibu wetu wa kushiriki kwenye Tabligh lakini wakati huo huo kushughulika na malezi ya wanajumuiya wakiwemo wapya na wakongwe pia.

Hivyo miongozo aliyowahi kutupatia Khalifa Mtukufu a.t.b.a. juu ya Tabligh na Tarbiyyat ni mingi mno, isiyowezekana kutajwa hata sehemu yake ndogo hasa katika dakika hizi chache na hivyo hapa chini nitaeleza baadhi tu ya nukuu chache zinazothibitisha kauli yangu kwamba Huzur Aqdas a.t.b.a. ameendelea kutukumbusha kwa namna mbalimbali juu ya wajibu wetu wa kuendeleza jihadi ya tabligh na tarbiyyat.

Sote tutakumbuka kwamba mwanzoni tu mwa kuchaguliwa kwake Huzur Aqdas alitupitisha tena kwenye maana ya Baiat, kupitia hotuba kadhaa za Ijumaa akayafafanua kwa mapana na marefu masharti kumi ya baiat na humo akatueleza wajibu wetu mwingi wa kufanya Tabligh na Tarbiyyat.

Nakuombeni sote tukisome kitabu kilichokusanya maelezo hayo ambacho kipo kwa Kiswahili kwa jina la Masharti ya Baiat na majukumu ya Muahmadiyya.

Kwa wale ambao hatujapata bahati ya kukisoma hata mara moja nakuombeni sana, tena sana tukisome kitabu hicho na kwa wale ambao tulishapata kukisoma nakuombeni tukipitieni tena na tena. Nakumbuka dada mmoja baada ya kukisoma kitabu hicho aliwahi kufika ofisini, machozi yakikaribia kumtoka na kusema natamani kila Lajna wa Tanzania asome kitabu hiki, naye akajitolea kiasi cha fedha ambacho kiliwezesha Lajna wa matawi kadhaa kupatiwa angalau nakala moja ya kitabu hicho. Ni imani yangu kwamba Lajna hawakuipuuza wala hawatoipuuza hisani hiyo waliyofanyiwa.

Kwa upande wa nukuu naomba nianze na hii ya hivi karibuni:

Kwenye salamu za Jalsa alizotutumia mwaka uliopita Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema yafuatayo:

"Nawahimizeni kusikiliza wakati wote hotuba zangu za Ijumaa pamoja na maelekezo na Hotuba zangu zingine. Hii itawawezesheni kuimarishika mshikamano na utii wenu kwa taasisi ya Ukhalifa. Mnapaswa pia kuwafundisha watoto wenu juu ya Baraka maalum za taasisi ya Ukhalifa na kuwahimiza kudumu wameshikamana nao, na kuwa siku zote watiifu kwa Khalifa wa zama. Leo hii, kazi ya kuhuisha Islam inaweza tu kufanywa kwa kushikamana na mfumo wa Ukhalifa. Kwa hiyo, inatakiwa daima mjitahidi kuienzi taasisi hii adhimu na kuhakikisha nyinyi na vizazi vyenu vijavyo, siku zote mnabaki katika mwongozo wenye baraka na hifadhi ya Khilafat-e-Ahmadiyya. Allah awawezesheni kufanya hivyo.

Nataka pia kuwakumbusheni wajibu wenu juu ya mahubiri. Tabligh ni lazima kwa kila Muislam Ahmadiyya na mfano wenu mwema ni wa lazima ili kupata mafanikio katika juhudi zenu za Tabligh. Kwa hiyo kama matendo yetu yataoana na mafundisho ya Islam na kila neno na tendo letu litaenda sawa na mafundisho ya Qur'an Tukufu, na yatakuwa katika umbo na hali ambayo Masihi Alieahidiwa (as) ametamani kwa ajili yetu, basi hii itakuwa ni nyenzo kubwa ya kupeleka ujumbe wa Islam Ahmadiyya kwa watu wa nchi yenu kimahsusi na dunia kwa ujumla. Allah na awabarikini wote!."

Kwenye hotuba yake ya terehe 31/01/2014, Huzur Aqdas Alisema yafuatayo juu ya mahusiano ya Tarbiyyat na Tabligh:

"Yapaswa kukumbukwa kwamba wakati elimu juu ya maswala ya kifo cha Yesu a.s. na umwisho wa utume ni ya muhimu – kwa ajili ya ustawi wetu wa mbele wa mapambano ya nje, ni muhimu sana pia vile vile kujenga matendo mema na elimu ya kumfahamu Mungu kwa ustawi wetu wa mbele wa mapambano ya ndani. Usafi wetu wa kiroho na sahihiko la mwenendo, Inshallah vitaleta mabadiliko ya kimapinduzi makubwa zaidi kuliko jitihada zetu za Tabligh.

Kauli ya Hazrat Musleh Mauud a.s. bila ya shaka ina uzito mkubwa pale aliposema: "Ikiwa watasahihisha nyoyo zao (maulamaa na wabashiri wa jamaat) na kutilia ufahamu na mapenzi ya Allah Mwenye enzi ndani ya nyoyo za watu hapo makumi ya mamilioni ya watu wataanza kuja kujiunga na Ahmadiyyat..... Ikiwa mtaeneza dini yenu kwa njia ya tabligh, hapo watu watawajieni katika umoja na uwili. Lakini, ikiwa mtaomba maghofira na kumtukuza Mwenyezi Mungu na kuondosha madhambi katika Jamaat, hapo watu kwa makundi makubwa watajiunga nanyi.

.... Hivyo yatupasa kuzingatia kusahihisha mwenendo wetu na tujitahidi tuwe wawakilishi wa Khilafat na tujitahidi tuwe wasaidizi wa Khalifa wa zama. Hatuwezi daima kuwa tunashughulika na mijadala ya kinadharia tu, bali yatubidi kuipeleka Jamaat yetu katika matendo na Inshallah kwa ajili ya hili tunahitaji kutumia njia nyingine nayo ni kusahihisha tabia. Kinachohitajika ni kuwa na matendo mema, kuwa na viwango vya juu vya ukamilifu na kutegemeka kutumia njia halali za kupata mapato. .... Wakati walimu wanapaswa kuzingatia hili, kila mwanajumuiya vile vile anahitaji kujitazama na kusahihisha tabia zake.

Katika hotuba yake ya tarehe 9 Aprili 2010 aliyoitoa mjini Pedro Abad, Spain, Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema: "Kazi ya kuihuisha Islam ni kazi ya kila Ahmadiyya. Kwa miniajili hiyo tunao wajibu mkubwa wa kutilia maanani hali zetu na kila mmoja afanye kazi kwa juhudi kulielekea lengo hilo." ..... Njia ya uhakika ya kusambaza imani ya kweli ni kupitia maendeleo ya kiroho na maendeleo ya kiroho hayawezi kufikiwa bila ya maombi na kuwa na maungano na Mwenyezi Mungu. Inawezekanaje basi kazi ya kuwaita watu kwa Mwenyezi Mungu ifanikiwe bila ya muitaji kwanza kuwa na maungano ya kweli na Mwenyezi Mungu? Masihi Aliyeahidiwa a.s. ametueleza kwamba ushindi wetu utakuja kupitia maombi. Tabligh pia inazaa matunda kupitia juhudi ya maombi yakichanganyika na juhudi maalum ya mtu kutengeneza mienendo yake.

Ndugu zangu wapendwa, Kama nilivyosema kwamba karibu kila hotuba ya Huzur Aqdas inatuelekeza kwenye Tabligh na Tarbiyyat, na kila hotuba inao uzuri wake, shani na umuhimu wake lakini katika hotuba kadhaa nilizozipitia, kwa maoni yangu sikuona hotuba ambayo ilikuwa na uzuri wa ajabu na shani ya kipekee kuliko ile ambayo Huzur Aqdas a.t.b.a. aliitoa juu ya ardhi hii, katika mkoa huu na katika wilaya hii kwenye siku kama hii, wakati akifunga Jalsa Salana yetu ya mwaka 2005 wakati alipotutembelea.

Huzur Aqdas a.t.b.a. alisema:

Leo ninyi ni maskini na wanyonge kwa sababu hamshindani katika kufanya mambo mema. Hivyo shindaneni katika mema ili muwe watu wa kurejesha heshima ya taifa lenu na kulifanya litajwe kwa wema duniani.

Kushindana katika mema maana yake mtekeleze amri zote za Mwenyezi Mungu.

.... Kumbukeni kwamba amali nzuri ni ile ambayo kila siku inaendelea kuboreka na kwa ajili ya kufikia ubora wake mtu anajitahidi kila siku. Haitakiwi kamwe iwe hivi kwamba muanze hatua moja ya wema na kisha msite hapo hapo kwenye ngazi ya kwanza kwa sababu kama mtasita hapo hamtaweza kamwe kukwea juu. Kwa mnasaba huu Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema:

Mtu anatakiwa afikie kushidana na wenzake katika kufanya mema. Kusimama kwenye kituo kimoja tu si sifa nzuri. Si mnaona maji yaliyotuama sehemu moja hatimae huchafuka, kwa sababu ya matope huanza kutoa harufu mbaya na kupoteza ladha yake? Bali maji yatembeayo daima huwa safi na huhifadhi ladha yake hata kama kwa chini yake kuwe na mchanga, lakini mchanga huo hauwezi kuyaathiri. Basi hivi pia ndivyo ilivyo hali ya mtu kwamba asikwame sehemu moja tu, kwani kukwama sehemu moja tu ni jambo la hatari sana. Daima inatakiwa hatua ipigwe kuelekea mbele. Mtu ajitahidi kukua katika matendo mema, vinginevyo hatopata msaada wa Mwenyezi Mungu.

Katika hali hii (ya kukwama sehemu moja) mtu hujinyima mwanga na hatimae hugeuka kuwa murtadi. Na mwishowe mtu kama huyu hupata upofu kwa ndani. Baraka na msaada wa Mwenyezi Mungu huwa pamoja na yule mtu tu ambaye daima hupiga hatua kwenda mbele na hakwami sehemu moja tu. Watu wa namna hii ndio hupata mwisho mwema. (Al Hakam, Vol.12 No.16 dated 2 March 1908 page 6).

Sasa angalieni jinsi Masihi Aliyeahidiwa a.s. alivyotukumbusha kwa uzuri kabisa juu ya haja ya kupiga hatua mbele za matendo mazuri. Nyote mnatambua juu ya hali ya maji ambayo husimama sehemu moja tu kwenye kidimbwi, kama mvua itanyesha mwanzoni hata vidimbwi vidogo au vibwawa huoenakana maji yake yako safi. Lakini kama mvua ikatike kwa kipindi kirefu basi maji yake huanza kuchafuka na haijalishi dimbwi lina ukubwa kiasi gani. Wadudu fulani huanza kuogelea kwenye dimbwi hilo na hatimae maji yanachafuka na kuchafuka zaidi. Magonjwa mengi pia huweza kupatikana kutoka kwenye maji hayo. Na kama kiangazi kitaendelea na mvua isinyeshe kwa kipindi kirefu basi mwishoni dimbwi hukauka kabisa.

Hivyo Masihi Aliyeahidiwa a.s. amesema kwamba hata kama mtu anafanya matendo mema lakini iwapo hajipatii faida ya mvua mpya kwa kupiga hatua mbele katika kuongeza mema yake, basi mtu kama huyo huwa ni sawa na maji yaliyotuama na atayafanya matendo yake mema ya kabla, yote kupotea, kwa sababu ya kusimama kwake mahala pamoja tu. Mazingira mabaya pia yatamuathiri.

Lakini maji yanayotembea ni maji ya mito ambayo maji ya mvua iliyonyesha karibuni hupata kuchanganyika na maji ya chemchem, na hata maji yayeyukuyo kutoka juu ya milima ya theluji pia huchangayika nayo. Kwa maneno mengine maji yatembeayo hupata kuchanganyika na maji mengine kutoka vyanzo mbalimbali. Na kila uelekeako mto wenye maji yanayotembea huzidi kutanuka, na kuwafaidisha viumbe wa Mwenyezi Mungu kila upitapo. Unawatimizia mahitaji yao. Na kila unapozidi kutembea unajisafisha takataka zake.

Hivyo mtu anayejitahidi kukuza matendo yake mema, naye pia hutanuka kila siku na anapata kufaidika na kazi njema za watawa na wachamungu wengine wanaomzunguka, anajitahidi kwa maombi na kwa msaada wa Mwenyezi Mungu kushikamana na mafundisho ya Quran Tukufu kama njia ya kukua katika mambo mema, na kwa sababu daima anakuwa na kiherehere cha kukua katika wema, basi Mwenyezi Mungu Naye anamshushia baraka Zake na fadhili Zake. Kisha mtu huyo kwa hakika anafikia kuwa kama mto utembeao ambao wanaadamu wanauthamini sana kwani wanapata manufaa yao kutokana nao. Uchafuzi wa mazingira hauwi na athari mbaya kwa mtu kama huyo.

Hivyo basi kila Ahmadiyya kama ulivyo mto utembeao anatakiwa daima ayafanye matendo yake mema kuwa yenye kukua. Kama tutafanya hivi sio tu kwamba tutajifaidisha wenyewe bali pia tutawafaidisha na wengine. Vinginevyo, kama Masihi Aliyeahidiwa a.s. alivyosema kama ninyi hamtokuza matendo yenu mema, mwishowe mtajiondoa wenyewe kutoka Ahmadiyat na Islam pia. Au kama yalivyo maji machafu ya dimbwi, mnaweza mkawa na chembechembe za dini lakini chembechembe hizo hazitokuwa na faida yoyote kwenu na kwa kizazi chenu kijacho. Kizazi chenu kitakuwa mbali sana na dini na kitakuwa mbali sana na mtendo mema.

Kila Ahmadiyya kwa hivyo, daima ajitahidi kusonga mbele katika matendo mema. Na ni hapo tu ndipo mtakapokuwa kama maji ya mto utembeao na kama ambavyo maji ya mto utembeao huwafaidisha wengine na ninyi pia ndipo mtakapoweza kuwafaidisha wengine. Mnatakiwa mjitahidi kuwafaidisha wengine. Na njia kubwa ya kuwafaidisha wengine ni hii kwamba ninyi muufikishe ujumbe wa Masihi wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w., ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambaye ni mtoto wa kiroho wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w.. Huu ni ujumbe ule ule ambao Mwenyezi Mungu aliushusha kwa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kwa ajili ya kusimamisha sharia.

Iwapo ninyi mtafanya matendo mema kwa namna hii na mtafuata sharia hii na mtafikisha ujumbe wa kutenda wema kwa wengine, basi fadhili na baraka za Allah zitakumiminikieni kwa wingi mno na matendo yenu mema yataongezeka na kukua zaidi. Mtaendelea kuwa karibu na Mwenyezi Mungu. Maji haya ya kiroho ambayo Mwenyezi Mungu amekunyeshelezeeni juu yenu ni jukumu lenu kuyabeba na kuyafikisha kwa wengine. Iwapo hamtoufikisha ujumbe huu, iwapo hamtoyafikisha kwa wengine maji haya ya kiroho ambayo mmeyapokea kutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s., basi mtakuwa mmejifungia kwa mikono yenu mlango mmoja mkubwa wa kukua katika wema, (Na mlango huo utabaki kujifunga) hadi pale mtakapowajali ndugu zenu na kuishika mikono yao na kuwakumbatia ili kwamba nao waanze safari ya kuelekea kwenye kutenda wema.

Ninyi mnayo asili ya wema miongoni mwenu na katika watu wenu wako ambao huathiriwa sana na matendo mema. Hivyo iwapo mtajitahidi katika nyanja ya Tabligh, mnaweza kuleta mapinduzi makubwa. Na hapo Inshallah, Mungu Apendapo, mtaweza kujiokoa ninyi wenyewe, mtaweza kukiokoa kizazi chenu, na mtaweza kuliokoa taifa lenu pia. Hivyo jitahidini kuelewa wajibu wenu.

Mwenyezi Mungu amjaalie kila Muahmadiyya, mwanamke na mwanamume, aliye mkubwa na aliye mdogo miongoni mwenu kuelewa wajibu wake na kujitahidi kusonga mbele katika matendo mema. Msifanye jambo lolote lililo kinyume na maslahi ya Jamaat na uzuri wake na ambalo halina manufaa kwa taifa lenu na pia msifanye jambo lolote ambalo halina maslahi mema kwa watu wa taifa lenu. Iwapo kwa kukanyaga kwenye njia zilizofundishwa na Mwenyezi Mungu, mtajaribu kutenda matendo mema na kuyakuza, basi hakutokuwa na jambo lolote la kuharibu heshima yenu, au litakalovunja heshima ya Jamaat au litakalolileta taifa lenu jina baya.

Jama'at Ahmadiyya Tanzania ilishawahi kutengeneza watu wengi wa namna hii ambao walikwea vilele vya juu kabisa katika matendo mema, ambao walipiga hatua katika utawa na ambao kupitia kwao hata jumuiya inajisikia fahari. Walilitumikia taifa lao. Miongoni mwa Waahmadiyya waliopita ni mfano wa Bw. Amri Abedi. Na natumaini kwamba watakuwepo wengi pia miongoni mwenu kwa siku hizi.

Iwapo mnatafakari na kujali kwamba khatima yenu iwe njema mtakapokutana uso kwa uso na Mwenyezi Mungu, ili kwamba muwe wavunaji wa radhi za Mwenyezi Mungu basi mfanye juhudi katika uchaji Mungu na pia mjitahidi sana kukuza amali zenu njema. Iwapo mtajipanga na kutenda sawa na mamarisho ya kimbingu basi kwa hakika mtastahili kuwa wapokeaji wa baraka Zake.

Mwenyezi Mungu ni Mbora wa watoaji na ambaye ni mwaminifu mno katika ahadi Zake. Mwenyezi Mungu humkimbilia yule anayetembea kuelekea Kwake. Hivyo iwapo kuna udhaifu wowote, basi eleweni kwamba udhaifu huo unatokana na ninyi wenyewe. Basi tujitahidi kuundoa huo.

Kumbukeni kwamba miongoni mwa kazi kubwa iliyo njema ni kuwa watiifu kwa taifa lenu pamoja na kulipenda. Kwa hakika sawa na hadithi moja ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w., mtu kuipenda nchi yake ni sehemu ya imani. Mwanajumuiya hatakiwi kuonesha Mapenzi ya nchi yake kwa maneno matupu tu, bali kwa matendo yake pia, na njia kubwa ya kuonesha mapenzi hayo kwa matendo ni kufanya amali njema. Kwa kushika mfano wa Waaminio wa kweli, ipelekeni nchi yenu safu ya mbele miongoni mwa mataifa.

Nchi yenu ni nchi kubwa, ni nchi nzuri, ni nchi yenye rutuba ambayo daima iko kijani. Ni nchi iliyo na utajiri mkubwa wa rasilimali. Nchi hii ilitakiwa iwe miongoni mwa nchi zilizoendelea duniani. Mwenyezi Mungu Akuwezesheni kulifanya hilo litokezee.

Daima kumbukeni kwamba Muahmadiyya ni mtu anayependa iwepo amani katika nchi yake na hivyo yafumeni maisha yenu yaendane sawa na sheria za nchi.

Mwenyezi Mungu Akusaidieni. Mwenyezi Mungu daima Akuongezeeni mapenzi yenu na utii wenu kwa Jamaat na Ukhalifa. Amin.

Uholanzi yapata Mabadiliko makubwa

Kutoka uk. 12

walikuwa Ahmadiya na maisha yao yameboreka baada ya kuja hapa wanapaswa kukumbuka kwamba wao wanao mzigo mkubwa wa deni wanalowiwa na Jumuiya kwa hili. Kama alama ya shukrani wanapaswa kujitahidi na kuleta mabadiliko ya kipekee yaliyo na Ikhlas kwao wenyewe na pia wanapaswa kuwaambia watoto wao neema ya Mungu iliyo juu yao na jinsi ambavyo wao na watoto wao wanavyotakiwa kwenda mbele daima kujaribu kutimiza ahadi ya Bai'at ambayo baba zao waliifanya.

Sisi sote pia tunao wajibu wa kuendelea kuwafundisha watoto wetu kuwa wenye shukrani kwa Mungu kwa ajili ya kutufanya sisi kuwa na hali bora zaidi kifedha baada ya kuja hapa na kuwaambia kwamba, katika kuonesha shukrani kwa fursa za kielimu na kitaaluma ambazo wamezipata wanapaswa kuwa na uhusiano mkubwa na Nizaam ya Jumuiya na maungano yaa uaminifu na utii kwa Ukhalifa. Kadhalika ni wajibu wa kila Ahmadia daima kuwa na uhusiano mkubwa na Nizaam na maungano yaliyohalisika ya uaminifu na utii kwa Ukhalifa ambao wamefunga nao ahadi wakati wa Bai'at.

Kwa neema ya M Mungu Waahmadiya wapya, hasa wale ambao wamekubali kwa imani kamili na ufahamu pamoja na kutafakari juu ya ahadi zao na masharti ya Bai'at wanajitambua na huwa wanamuandikia Huzoor kuhusu hili. Hata hivyo, wengine wengi ambao ni Ahmadiyya wa kuzaliwa au wale ambao wazazi wao wamekubali Ahmadiyya walipokuwa watoto na wao hasa wanapendelea zaidi masuala ya kidunia masuala na wala hawatafakari kwa ujumla juu ya hali yao ya Bai'at wala hawafahamu kiapo cha Bai'at wala si wenye kukumbuka neema ya Mungu juu yao kutokana na wao kuwa Ahmadiya. Hii inatokea licha ya tukio la Bai'at kutangazwa MTA mara kwa mara. Hawafanyi jitihada za kuzingatia umuhimu wa Bai'at na kuiweka katika vitendo na wao pia hawafanyi juhudi ipasayo kufanywa katika kukuza maungano na uhusiano wao na Ukhalifa. Na hii si tu kuhusu wale ambao waliomba hifadhi ya kisiasa lakini hii inahusika na Ahmadia wote. Mfano wa wanaotafuta hifadhi ulitajwa kabla kwa sababu wengi wa walipo kwenye sala hii kwa sasa ni wa wale ambao walitaka hifadhi na hivyo kupata nafuu kwenye maisha yao, vinginevyo Ahmadiya wa namna hii wanaweza kupatikana katika sehemu zote za Jumuiya duniani. Iwapo kila mtu binafsi atajitathimini ataweza kuona mahala aliposimama. Hali hii ya kujitafakari na kujichunguza binafsi inatakiwa isiwe ya juu juu tu na ya haraka haraka, badala yake kila mmoja anapaswa kutafakari kwa kina juu ya hali yake na itakuwa ni jambo la maana kama atamalizia katika kuona mapungufu yake na kama si hivyo, juhudi zinapaswa kufanywa ili kutengeneza hali zetu binafsi.

Katika sharti lake la kumi la Bai'at Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alitangaza: Kwamba Katika ahadi ya udugu, atakayofungamana nami (Masihi niliyeahidiwa) kwa sharti ya kutii kila amri njema, atatimiza ahadi hii mpaka kufa kwake na katika ahadi hii ya udugu ataonesha utii na unyenyekevu wake kwa imara zaidi kuliko ufungamano wowote, wa damu au wa bwana na mtumishi.. '

Maneno haya yanaweka wajibu mkubwa juu yetu wa kuwa na upendo uliohalisika kwa Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake). Hapa, yeye anachukua ahadi kutoka kwetu kuwa kwa ajili ya M Mungu sisi tutaanzisha viwango vya hali ya juu vya upendo, mapenzi na mafungamano ya udugu na kuthibitisha daima kuwa watiifu katika kila uamuzi mzuri, kila kitu ambacho Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alikuwa amefunuliwa katika mwanga wa mafundisho ya Uislamu. Na utii huu utakuwa si tu wa kipindi kifupi lakini tunatakiwa tujaribu kudumu nao mpaka pumzi yetu ya mwisho. Na maungano haya yatakuwa yasiyo na mfano miongoni mwa mahusiano mengine yoyote ya kidunia, ikiwa ni pamoja na mahusiano ambayo sisi tunayaunda kwa uaminifu na pamoja na mahusiano ambayo sisi tunayaunda kama shukurani kutokana na mema tunayofanyiwa na wengine. Kama kuna uwezekano wa kuwa na kiwango cha juu cha upendo kwa mtu yeyote baada ya Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake) inatakiwa iwe ni kwa mtumishi wake wa kweli na mkereketwa, Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake). Kila mtu anaweza kuchambua ni kwa jinsi gani unapaswa kuwa uhusiano wetu na Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) katika mwanga wa hili. Je, hivi ndivyo viwango vyetu kwa pamoja pamoja au sisi tunavisahau viwango hivi kwa mtazamo wa maslahi yetu binafsi? Je, mambo ya kidunia yanatufanya kuondokana na upendo huu na utii?

Mtu hufanya vitendo kwa faida au kutokana na hofu, hofu ya ya kuulizwa au kwa sababu ya upendo na usafi. Wale ambao wana ufahamu sahihi wa imani hufanya matendo kwa upendo na uaminifu. Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) anatarajia sisi kuongeza hali hii baada ya kuchukua kwetu Bai'at. Kama hali yetu haitokuwa hii basi ushauri wowote unaotolewa hautokuwa na athari yoyote. Je, kuna Ahmadiya yoyote anayeweza hata kufikiria kwamba Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alisema chochote kilicho kinyume na Qur'ani Tukufu na Sunna? Bila shaka hakuna. Kwa hiyo, kila Ahmadia anapaswa kuelewa kuwa 'utii katika kila kitu vizuri' maana yake ni kuwa mtiifu kikamilifu baada ya kukuza upendo wake kwa (MA) kwa kiwango cha juu na kisha kuangalia kila mafundisho. Ni lazima sisi kuangalia kila upande ni kipi Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) anakitarajia kutoka kwetu na kile yeye alichotuelekeza. Vinginevyo huduma yetu itakuwa ni ya mdomo tu. Kama hatujui hata ni nini Masihi Aliyeahidiwa alisema, inakuwaje tuweze kumfuata? Sisi pia tunatakiwa kama Waahmadia kuongeza ufahamu wetu na kutekeleza kile tulichoelekezwa kwa uaminifu. Ushauri na maelekezo ya Masihi Aliyeahidiwa ya (amani juu yake) yanaweza kupatikana katika vitabu vyake mbalimbali na matamko. Huzur alisema atwasilisha maandiko machache kati ya haya.

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alisema: Jumuiya yetu haipaswi kuishia kwenye maneno tu bali inapaswa kutimiza lengo la kweli la Bai'at kwa matendo. Mabadiliko ya ndani ni lazima yapatikane kwa sababu hatuwezi kumfurahisha Mungu Mwenyezi kwa hoja tu za maneno. Kama utashindwa kuleta mabadiliko ya ndani basi hakuna tofauti kati ya wewe na wengine.

Pia alisema: Kila mtu anapaswa kufanya juhudi binafsi katika kutimiza ahadi yake.

Kumuamini Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) katika ngazi ya mafundisho na kukubali ukweli wake na kunyamazisha wengine kwa hoja si kitu chochote kama matendo yetu si sahihi.

Alisema: "Fanyeni juhudi kuleta mabadiliko ndani yenu. Kwa maombi wakati wa Swala, kutoa sadaka, na kutumia njia nyingine zote ili kufikia kuwa miongoni mwa wale: "Na kwa wale wanao jitahidi katika njia yetu ... ' (29:70) Na hili linaleta matokeo '... Sisi tutawaongoa kwenye njia zetu ...' (29:70)

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) pia alisema: "inawezekanaje kwamba mtu ambaye hajali na ni mzembe aweze kupata ukarimu wa Mungu kama vile mtu ambaye anatumia akili zake zote, nguvu zake na uaminifu katika kumtafuta? '

Wakati Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) aliposema tumfuate na kuwa mtiifu kwake, ni kweli kwamba kwa njia yake sisi tutapata njia ya kumuona Mungu na kuwa wenye kujichumia neema za Mungu. Hivyo tunatakiwa tuwe miongoni mwa wale ambao wanasimamisha Salat kwa wakati na kwa masharti yake na pia kutoa michango yetu na sadaka zingine ili kuvutia upendo wa Mungu kwetu.

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alisema: Daima Kukumbukeni juu ya mambo mawili. Kwanza, kuwa mifano ya Waislamu wa kweli na pili, kueneza sifa njema za Uislamu katika dunia.

Kama sisi wenyewe hatuna elimu ya kutosha na kama matendo yetu yanatia wasiwasi tunawezaje kuwa mifano ya kweli ya Uislamu na jinsi gani tunaweza kuzungumzia uzuri wa Uislamu?

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alisema kuwa Jumuiya inapaswa kuchukua umakini sana kama wana haki au la.

Tunapaswa wote binafsi kutafakari iwapo tuna muegemeo zaidi kwa dunia au kwa manufaa ya imani, wote sisi wenyewe na kwa watoto wetu. Je, tuna hofu ya Mungu na iwapo tunafanya jitihada za kufikia radhi zake?

Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) pia alisema: Kuepuka ghadhabu zisizo za haki na kuepuka hasira pia ni tawi la Uchamungu.

Wale ambao wana mwelekeo huu ni lazima kutafakari juu ya hali yao.

Kama tutaendelea kushika ushauri huu wa Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) na kuuweka daima mbele yetu na kuutafakari tena na tena, huo utaongeza upendo wetu na maungano yetu Kwake. Hakika, yeye alikuwa na maumivu sana juu ya hali ya kiroho ya Jumuiya yake. Alikuwa na wasiwasi zaidi kuliko baba na mama katika suala hili na kwa kurudi rudia alitushauri ili kutuepusha na njia za upotofu na kutuweka katika njia iliyo sahihi. Baada ya kusoma kuhusu usemi huu wa upendo na sababu ya wasiwasi wake kwetu hakuna sababu kwa Ahmadia yoyote kutokufikia viwango hivi vya juu vya maungano na utii kwa Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake).

Ni fadhili ya Mungu juu yetu kwamba baada ya Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) Yeye Ameanzisha Ukhalifa kati yetu na Ukhalifa lengo lake ni kuendeleza na kukamilisha kile ambacho Mungu alimtuma nacho Masihi Aliyeahidiwa. Kwa hiyo, kwa kujitahidi kukuza maungano yaliyohalisika na utii kwa Ukhalifa tunaweza kuendelea na safari yetu ya [kiroho]. Kama Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) alivyosema tunapaswa kuonyesha mifano ya Waislamu wa kweli na kueneza ujumbe wa uzuri wa Uislamu.

Ahmadia wanachukua ahadi ya Bai'at kwa mkono wa Khalifa wa zama na hivyo ni muhimu kutimiza ahadi hii. Kwa hiyo, ushauri, maelekezo na mipango inayotolewa na Ukhalifa inapaswa kutekelezwa ili kutimiza ahadi hii. Kila Ahmadi anashika ahadi wakati wa Bai'at kutekeleza kwa kudumu masharti ya Bai'at na kumtii Khalifa wa zama katika kila amri njema. Kazi ya Khalifat e Ahmadiyya ni kuendeleza kazi ya Masihi Aliyeahidiwa. Iwapo tutazingatia hili, viwango vya kweli vya utii vitaweza kuimarishwa na kutakuwa na umoja na fursa nyingi za Tabligh zitaweza kufungua.

Hata hivyo, kama kila mtu anatangaza kwamba yeye amempokea Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) na anayo maungano naye lakini kisha akaendelea kushika njia yake mwenyewe, hakutakuwa na maendeleo yoyote. Uzuri wa Jumuiya upo pamoja na Ukhalifa. Na uhusiano wetu na Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) ni kwa mujibu wa yeye kuwa mtumishi wa kweli na mkereketwa kwa Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake), na hivyo tuna wajibu pia wa kupanua maungano haya kwa Ukhalifa.

Siku chache zilizopita wakati wa dhifa baada ya uwekaji wa jiwe la msingi la msikiti Hazrat Khalifatul Masih alitoa hotuba fupi kwa kuzingatia mafundisho ya Uislamu, umuhimu wa misikiti na majukumu ya Ahmadiya. Mgeni mmoja mwanamke aliyealikwa katika dhifa hiyo alisema kuwa maneno ya Khalifatul Masihi yalikuwa makubwa, sasa kinachobakia kuonekana ni kwa kiasi gani Waahmadiya watayaingiza maneno haya kwenye matendo yao katika kujenga mazingira ya upendo na amani. Hakika, Ahmadiya wanaoishi katika eneo hili sasa wapo chini ya uchunguzi. Wanahitaji binafsi kutafakari kwamba ili kufanikiwa kwenye uchunguzi huo waongeze juhudi kubwa ya kufuata maagizo ya Khalifa. Kwa hiyo, haitoshi tu kufanya kiapo cha Bai'at. Matendo mazuri yanahitajika kwa ajili ya matengenezo yetu wenyewe na pia kwa ajili ya Tabligh. Ili kuwa na umoja na mshikmano katika kila mahali na juu ya kila ngazi inahitajika kwamba sisi tufuate ishara ya mkono mmoja tu; yaani katika kutii Ukhalifa.

Ni neema kubwa ya Mungu kwamba Jumuiya inawezeshwa kutumia teknolojia ya kisasa, TV na intenate kwa ajili ya uenezi wa imani. Vitabu na maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) yanapatikana kwa wingi kwenye tovuti yetu na yanaweza kupatikana wakati wowote mtu anapotaka. Pia kazi zake zimetafsiriwa katika lugha kuu za dunia. Kadhalika, miongozo ya Khalifa wa zama pia inaweza kusikilizwa na kusomwa nayo ipo juu ya msingi wa Qur'ani, hadithi na maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake). MTA inatangaza ujumbe wa Islam duniani kote na hii inaipatia Jumuiya hisia mpya za umoja. Tunapaswa kila mara kusikiliza MTA ili kuwa sehemu ya umoja huu. Kwa uchache sana angalau hotuba ya Ijumaa ni lazima kusikilizwa kila wiki kwa umakini maalum. Kila familia inapaswa kuona kama kila mwana familia wao amefanya hivyo. Kama mke anasikiliza lakini mume hasikilizi , itakuwa haina maana yoyote. Na hivyo hivyo ama mume anasikiliza lakini mke na watoto hawasikilizi, pia itakuwa haina maana yoyote. Kila Ahmadia anapaswa na inabidi awe sehemu ya utaratibu huu ambao M Mungu Ameuweka ili kuwezesha zaidi umoja na kwa njia ambayo sauti ya Khalifa wa zama inafika kila kona ya dunia. Umakini mkubwa wanapaswa kutolewa kwa hili. Kama hatujui kile ambacho Khalifa wa zama anakiagiza tutawezaje kuwa watiifu kwake? Iwapo sisi tutakuwa tunasikiliza maagizo yake tutakuwa na uwezo wa kutekeleza na kutii. Inabidi daima tuwe na hamu na jazba ya kuona nini Khalifa anataka tutekeleze na kutii. Vinginevyo tutakuwa tunafanya maigizo na usanii tu kwa kuahidi kila Ijtema au wakati wa Bai'at 'Kwamba tutatii kila amri njema' au 'tutajitolea kila aina ya muhanga kwa kuendeleza Ukhalifa wa Kiahmadiyya. "

Namuomba M Mungu ajaalie hivyo kwamba kila familia itoe kipaumbele kwa suala hili na ifanye matumizi kamili ya kituo hiki - MTA ambacho tumepewa kwa ajili ya tarbiyyat (mafunzo maadili). Kituo hiki sio tu rasilimali kwa ajili ya tarbiyyat, bali kimebeba jukumu kubwa katika kueneza mafundisho ya Uislamu. Kama kwa sababu fulani za kimaisha matangazo hayewezi kuangaliwa moja kwa moja, basi daima kuna rekodi za programu hizi na zinarejewa rejewa na pia zinaweza kuonekana kwenye mtandao.

Wakati taratibu hizi zinakuza maungano yetu na Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) pia zinaweza kuyapa nguvu maungano ya kila mtu na Ukhalifa na kumfanya aoneshe mifano ya utii. Kwa mujibu wa hadithi ya Mtukufu Mtume (rehma na amani za Mwenyezi Mungu iwe juu yake), utii huu uende hadi kwenye utii wa Mtume na kutupeleka kwenye utii wa Mungu na kufanya kila ktu katika kutafuta radhi yake. Naomba Mungu kuwawezesha kila mmoja kufanya hivyo!

Mwisho.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Muharram/Safar 1437 AH | OKT./NOV. 2015 | Tbk./ Nub. 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Huraira r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Hakuna yeyote anisaliaye isipokuwa Mungu atanirudishia roho yangu ili nimrudishie salamu yule mwenye kunisalia (*Abu Daud*)

Uholanzi yapata Mabadiliko makubwa

Na Mwandishi Wetu

Huzur alitoa hotuba ya Ijumaa iliyopita kutokea Masjid Noor Nunspeet, Uholanzi.

Baada ya Tashahud, Taaudhu na Suratul Faatiha kama ilivyo ada, Huzur alisema:

Wengi wa Waahmadiya waishio hapa ni aidha wale waliozaliwa ndani ya Ahmadiya au wale ambao familia zao ziliikubali Ahmadiyya tangu wao wakiwa watoto wadogo sana na hivyo ni kama vile wamekulia katika mazingira ya kiahmadia. Pia, wengi wa watu hawa ni wenye asili ya Pakistan ambao wanaishi hapa na wamepatiwa uraia wa nchi hii kwa sababu kwa kuwasili kwao hapa wao walisema kuwa walikuwa hawapewi uhuru wa dini kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu nchini Pakistan. Baadhi ya watu hawa walikuwa moja kwa moja wanakabiliwa na kesi mahakamani [nchini Pakistan]. Hivyo, idadi kubwa ya watu hapa wamepatiwa ruhusa ya kuishi kutokana na huruma ya serikali ya [Uholanzi] kwa sababu wao wamejitangaza wenyewe kuwa Ahmadiya. Tangazo hili la kuwa kwenu Ahmadia linaweka wajibu mkubwa juu yenu. Wale Ahmadiya ambao wamekuja hapa kwa mujibu wa utaalamu wao au fani nyingine yoyote na wanahusishwa na Jumuiya pia nao hawawezi kujitoa kwenye jukumu hili. Waahmadiya wapya ambao kwa kushawishika na ukweli wa MA wameamua kujiunga na jumuiya, pia nao wana wajibu wa kutimiza haki yao ya Bai'at. Mbele ya Mola wao waelewe kwamba hawatosamehwa watakapoendelea kufanya makosa kwa madai kwamba walifanya hivi na vile kwa sababu waliwaona waahmadiyya wa muda mrefu wakifanya hivyo.

Ni muhimu kuelewa ufafanuzi na maelezo ya Masihi Aliyeahidiwa (amani juu yake) juu ya Qur'ani Tukufu na Sunna. Ni muhimu kujifunza haya na imekuwa rahisi kwani yanapatikana sana na hakuna mtu yeyote mwenye udhuru wowote juu ya hili. Hazrat Khalifatul Masihi akawaambia Ahmadiya wa muda mrefu waelewe kwamba watakuwa dhima (kushiriki kwenye kosa) kama kuna mtu atajikwaa kwa sababu ya matendo yao. Kwa neema ya Mwenyezi Mungu wale ambao baba zao



Masjid Noor Nunspeet, Uholanzi, uliofunguliwa hivi karibuni.

Endelea uk. 11

Muongozo wa Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. juu ya Tabligh na Tarbiyyat

Hotuba iliyotolewa kwenye Jalsa 2015 na
Mwl. Abdulrahman M. Ame

Muongozo wa Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. juu ya Tabligh na Tarbiyyat

Sifa zote njema zinamthibitikia Allah ambaye kwa fadhili zake zisizo mipaka Ametuwezesha kukusanyika kwa mara nyingine kwa ajili ya Jalsa salana ya 46 ya nchi yetu, Tanzania.

Mada niliyopangiwa inahusu Muongozo/Maagizo mbalimbali ya Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. juu ya Tabligh na Tarbiyyat.

Ndugu zangu wapendwa, sisi ni watu tulio na bahati kubwa mno. Kwa kujaaliwa kumtambua na kumkubali kwetu Masihi Aliyeahidiwa a.s. tumejiweka chini ya mwamvuli wa wa baraka na msaada mkubwa wa Mwenyezi Mungu. Tumejiweka chini ya Ukhalifa wa Mwenyezi Mungu uliohaidiwa ndani ya Quran Tukufu, na ulioahidiwa ndani ya hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kutokea katika zama zetu hizi.

Akitaja kazi za Ukhalifa huu, Mwenyezi Mungu anasema ndani ya Quran Tukufu.

... na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea... (24:56).

Hivyo kwa mujibu wa aya hii miongoni mwa kazi kubwa ya Ukhalifa au ya Khalifa wa Mwenyezi Mungu ni kuimakinisha dini, ni kuiimarisha dini kwa kuwalea waaminio, mithili au zaidi ya mama akileavyo kichanga chake.



Mwl. Abdulrahman Ame, akitoa hotuba kwenye Jalsa Salana 2015

Wako watu ambao huuliza kwa kebehi, Khalifa leo ni wa kazi gani wakati ambapo Wanaulamaa wako wengi na wametajwa kuwa ni warithi wa Manabii.

Tunachoweza kuwakumbusha watu hawa ni hiki tu: Ni kujingikiwa kukubwa kulioje kwa mgonjwa kutokutambua kwamba anaumwa. Wanaulama waliotajwa kuwa ni warithi wa Manabii ni wale tu waliopo chini ya Ukhalifa, kwani hao ndio ambao hupata kulelewa asubuhi na jioni, kwa maana bila malezi hakuna kitu, bila malezi hakuna elimu, bila malezi hakuna imani, bila malezi hakuna dini, bila malezi ni dunia tupu, bila malezi ni kiza kitupu, kiza totoro! Hata Manabii wenyewe hawakuachwa na Mwenyezi Mungu hata dakika moja, waliendelewa kulelewa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe hadi walipoaga dunia.

Hivyo wakati ambapo Mwenyezi Mungu Mwenyewe anawalea Manabii, nao wanawalea wafuasi wao, Mwenyezi Mungu akakadiria kwamba baada ya Nabii kuondoka Ukhalifa chini ya misingi ya Unabii uendeleze ulezi huu kwa wafuasi wa Nabii husika.

Hivyo nirejee kusema kwamba kwa kuwakwetu chini ya Ukhalifa tunayo dhamana ya kubaki kwenye muongozo, kwani daima tunapata kulelewa, tunapata kukumbushwa, wajibu wetu na majukumu yatupasayo.

Makhalifa wa Mwenyezi Mungu ni hazina kubwa miongoni mwa hazina alizoziumba Mwenyezi Mungu na kama asemavyo Mwenyezi Mungu:

Na hakuna kitu chochote ila tunayo hazina yake, wala Hatukiteremshi isipokuwa kwa kipimo maalumu" (15:22).

Basi kila Khalifa ana shani yake, na Mwenyezi humjaalia vipaji sawa na haja ya wakati.

Katika wakati wetu tulionao, ambapo Jumuiya inapanuka kwa kasi duniani kote, sasa ikiwa imejikita katika nchi 207, huku tukishuhudia maendeleo makubwa ya teknolojia ya habari na mawasiliano ambapo wanadamu wanaweza hata kuwasiliana wote kwa dakika chache tu, lakini kwa upande mwigine tukikabiliwa na changamoto kadhaa zitokanazo na maendeleo hayo, swala la malezi ya wanajumuiya ni muhimu sana kabisa. Bali ni muhimu pia kwa wanajumuiya kupata miongozo ya jinsi ya kutekeleza majukumua yao ikiwemo kufanya Tabligh sambamba na teknolojia hiyo ya mawasiliano.

Ndugu zangu wapendwa, ninaweza kusema bila wasiwasi kwamba Kiongozi wetu Mpendwa, Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. tangu kuchaguliwa kwake hakuna jambo aliloendelea kulisisitiza zaidi na zaidi kuliko Tabligh na Tarbiyyat.

Tangu hotuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kwake

Endelea uk. 10